# Nipashe

Ijumaa Mei 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580226

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Spika awataka wabunge Chadema kurejea au mishahara yao kuathirika

UK. 8




UKURASA 11

# Corona yapoka tril. 2.5/- za utalii

## 470,000 kupoteza ajira, Tanapa, Ngorongoro, Tawa hali tete kimapato...

*Endelea uk. 2*



Watalii wakitembelea moja ya maeneo ya hifadhi za wanyamapori nchini. Juu ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamis Kigwangalla. **PICHA: MAKTABA**.

## ...Ewura kuwarejeshea maji wote waliokatiwa huduma

UK. 2

## BAA LA CORONA



Shirika la Afya Duniani (WHO), linatahadharisha kuwa uvaaji wa barakoa siyo kinga pekee ya kujikinga na virusi vya corona. Kuosha mikono mara kwa mara na kuepuka mikusanyiko ni mambo ya kuzingatiwa kila siku.

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## WABUNGE WALIOKO DAR WAITWA POLISI

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


**MICHEZO** MKUDE AIWEKA SIMBA MTEGONI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Corona yapoka trilioni 2.5/- za utalii

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amesema homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona imeathiri kwa kiwango kikubwa sekta ya utalii kimapato na ajira.

Kutokana na baa hilo, waziri huyo amebainisha watalii wamepungua, huku mapato yatokanayo na sekta hiyo yakitarajiwa kupungua kwa takribani Sh. trilioni 2.5.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Dk. Kigwangalla alisema sekta hiyo imeathirika kwa kiasi kikubwa kwa kuwa inategemea wageni kutoka nje ya nchi na sasa safari hazipo tena.

Alisema madhara haya yanaonekana kuwa makubwa zaidi na tayari kuna dalili za kushuka kwa mapato yaliyotarajiwa kukusanywa na taasisi kubwa zilizo chini ya wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Wakala wa Misitu (TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa).

Waziri Kigwangalla alisema kwa mwaka 2020/2021 Tanapa inalenga kukusanya jumla ya Sh. bilioni 363.9, lakini kutokana na hali inavyoendelea, makisio sasa yanakadiriwa kuwa Sh. bilioni 64 au chini ya hapo.

Kwa upande wa Ngorongoro, ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 162.7, kutokana na athari hizo zitakusanywa Sh. bilioni 58.

Alisema TFS ilikadiria Sh. bilioni 153.6 na sasa zitakusanywa ni Sh. bilioni 121, huku Tawa iliyokadiria kukusanya Sh. bilioni 58.1, sasa itakusanya Sh. bilioni 22.

"Kama hali itatulia mwezi Oktoba mwaka huu, idadi ya ajira za moja kwa moja katika sekta ya utalii itashuka kutoka 623,000 hadi kufikia 146,000," alibainisha.

Dk. Kigwangalla pia alisema watalii watashuka kutoka 1,867,000 waliotarajiwa hadi kufikia watalii 437,000, huku mapato yanayotokana na utalii yakitarajiwa kushuka kutoka Sh. trilioni 2.6 hadi kufikia Sh. milioni 598, ikiwa ni anguko la Sh. trilioni 2.5.

"Upungufu huo wa mapato ni mkubwa kwa sekta na unaweza kusababisha baadhi ya taasisi za uhifadhi zilizo chini ya wizara kushindwa kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara," alisema.

Waziri huyo alisema katika kukabiliana na hali hiyo, wizara imeendelea kuwashirikisha wadau wa sekta ili kuweka mikakati ya namna ya kuisaidia sekta isiathirike zaidi.

Alibainisha kuwa masoko makuu ya utalii ni katika mabara ya Ulaya, Amerika na Asia ambayo yamechukua hatua mbalimbali za kudhibiti kusambaa kwa corona.

Dk. Kigwangalla alisema hatua hizo zinajumuisha kuzuia raia wake kusafiri na baadhi ya mashirika ya ndege kutofanya safari nje ya nchi, hali iliyosababisha kuathirika kwa sekta hiyo, na kwamba ugonjwa huo umeleta madhara makubwa katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

"Sekta ya utalii kabla ya madhara hayo ilikuwa inachangia asilimia 25 katika mapato yote ya kigeni inayopata nchi yetu. Sekta hii imeathiriwa zaidi kutokana na ukweli kwamba inategemea zaidi mapato ya watalii wanaotoka nje ya nchi ambao kwa sasa kutokana na corona, wameshindwa kusafiri na wengi wao wamesitisha safari za kuja nchini kutalii," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri Kigwangalla, baada ya kuona madhara ya awali, wizara ilifanya tathmini ya awali (rapid assessment) iliyojikita katika kipindi cha tangu ugonjwa huo uanze hadi Aprili 6 mwaka huu (juzi) na kubaini athari hizo.

"Madhara makubwa ya corona katika sekta ya utalii yalianza kuonekana mwanzoni mwa Machi 2020, tofauti na miezi ya Februari na Januari 2020 ambayo hali ilikuwa shwari.

"Tathmini imebaini kuwa mashirika 13 ya ndege yalisitisha kuja nchini tangu Machi 25 mwaka huu na hivyo kuondoa uwezekano wa kuendelea kupata watalii kutoka nje ya nchi.

"Mashirika yaliyositisha safari zake ni pamoja na Emirates, Swiss, Oman Air, Turkish, Egyptian Air, South African Airways, Rwandair, Qatar, Kenya Airways, Uganda Airlines, Fly Dubai na KLM na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) nalo lilisitisha safari za nje," alisema.

Waziri huyo alisema kutokana na corona, fursa za kutangaza utalii hazitakuwa na matokeo chanya kwa sababu ya zuio la wageni kusafiri kutoka nchi moja hadi nyingine.

"Hali hiyo itasababisha kupungua kwa idadi ya watalii, mapato na kuathiri soko la ajira na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii," alibainisha.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella (katikati), akipokea msaada wa vifaa vya kujikinga na corona kutoka kwa Mhandisi Mtendaji Mkazi wa Kampuni ya Tanga Cement, Benedict Lema (kushoto), vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20, jijini Tanga jana. Kulia ni Katibu Tawala Mkoa huo, Judica Omari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Waliokatiwa maji kurejeshewa huduma kisa tishio la corona

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WIZARA ya Maji imeagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), kuwarejeshea huduma za maji wateja wote nchini waliokatiwa huduma hiyo kwa makubaliano.

Lengo ni kuwawezesha kupata huduma hiyo katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa COVID 19), ambao unasababishwa na virusi vya corona.

Aidha, Ewura kuhakikisha inadhibiti bei za ankara ya maji nchini zinazopandishwa kiholela na kubambikiwa wateja zinazofanywa mamlaka za maji nchini bila kupata kibali kutoka Mamlaka hiyo sambamba na kutoa elimu kwa Agizo hilo lilitolewa jijini hapa jana na Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso, wakati akizungumzia masuala mbalimbali na menejimenti ya Ewura, yakiwamo malalamiko ya ankara kubwa za maji zinazotolewa kwa wateja.

Alisema taifa liko katika mapambano na vita dhidi ya corona, hivyo jambo muhimu ni kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu.

Aweso alisema silaha pekee ya kukabiliana na maambukizo ya virusi hivyo ni maji tiririka na kunawa kwa sabuni.

Alisema kutokana na umuhimu wa maji, anaagiza wateja wote waliokatiwa maji warejeshewe kisha Uwura iweke utaratibu mzuri wa kulipa madeni yao.

Alisema licha ya mambo mazuri na kazi kubwa inayofanywa na Mamlaka hiyo, bado kuna matatizo na changamoto ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kutoa huduma bora kwa wananchi na hasa masikini.

Alieleza kuwa, zipo mamlaka za maji ambazo ni vinara kwa kuwabambikia na kuwapandishia wananchi bei za maji kiholela, hivyo aliiagiza Ewura kuhakikisha inafikisha ripoti ya mamlaka za aina hiyo wizarani ili kuzichukulia hatua stahiki, kwa kuwa wizara ndiyo yenye mamlaka ya mwisho.

Kadhalika, aliwataka watumishi wa Ewura kutoa elimu kwa watumiaji wa maji, juu ya wajibu na haki yao, hatua aliyosema itasaidia kuondoa malalamiko tofauti na sasa ambapo wateja wanapata haki ya kutumiwa ankara kwa njia ya simu bila ushirikishwaji.

Alifafanua zaidi ya kuwa kazi ya Ewura si kusimamia ankara pekee, bali ina wajibu wa kusimamia ubora wa maji ambayo lazima yawe safi na yenye ubora.

Kaimu Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira, Titus Safari, alisema Ewura, imetoa jumla ya leseni 119 katika kipindi cha Juni 2019.

Alisema, imekuwa ikifanya ukaguzi kwa mamalaka za maji nchini zisizopungua 50, na kutoa maelekezo ya kuboresha na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma Bora kwa watumiaji wa maji.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Godfrey Chibulunje, alisema maagizo yote yanayotolewa na wizara, likiwamo kurejesha huduma ya maji kwa waliokatiwa huduma watayafanyia kazi haraka iwezekanavyo.

## HABARI KITAIFA

# Fisi wazururaji kutegewa mbuzi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKURUGENZI wa Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, amesema kutokana na kushindikana kukamatwa fisi wanaozurura ovyo kwenye maeneo ya makazi ya watu, sasa wameandaa mtego wa mbuzi kuwakamata.

Alisema hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Manispaa ya Shinyanga, wakati Diwani wa Ngokolo, Emmanuel Ntobi, alipohoji hatua zinazochukuliwa na halmashauri kudhibiti wanyama hao ambao ni tishio kwa wananchi.

Alisema hatua walizochukua awali za kuwakamata fisi hao ni kuandamana na maofisa wa Maliasili, Idara ya Mazingira, Polisi na wanyamapori, lakini ilikuwa vigumu kwa sababu hawakuonekana. Hata hivyo, alisema walipoondoka fisi hao walionekana na wameamua kuwaandalia mpango wa kuwatega kwa mbuzi.

"Kumekuwapo na hadithi nyingi kuhusu fisi hao, tukienda kuwakamata hawaonekani, lakini tukiondoka wanaonekana, hivyo mkakati uliopo kwa sasa ni kununua mbuzi na kuwafunga kamba mahali wanapopita, pamoja na nyama zenye dawa ili wakiwavamia, hapo hapo tunawakamata," alisema Mwangulumbi.

Naibu Meya wa manispaa hiyo, John Kisandu, alisema matukio ya fisi kutishia usalama maisha ya wananchi ameyasikia na kuomba uongozi wa halmashauri uchukue jitihada za kuwaondoa wanyama hao.

Diwani wa Ngokolo, Ntobi, wakati akiwasilisha taarifa ya Kata yake katika eneo la usalama, alisema wananchi wake hawana amani kutokana na wanyama hao kuzagaa ovyo kwenye makazi yao na kutishia usalama wao.

Katika Mkoa wa Shinyanga yameshatokea matukio matano ya wananchi kujeruhiwa na fisi, huku mtoto mmoja Sungwa Kulwa (3), mkazi wa kijiji cha Dodoma, Kata ya Masanga, wilayani Kishapu mkoani humo, kufariki dunia baada ya kushambuliwa kichwani na fisi hao.

# Wabunge walioko Dar waitwa polisi

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kutoa saa 24 kwa wabunge walioopo mkoani kwake kwenda Dodoma, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewataka watunga sheria ambao hawajatii agizo hilo wajisalimishe ili wahojі.

Juzi, Makonda alitoa saa 24 kwa wabunge wote walioko mkoani kwake kurejea Dodoma, vinginevyo watakamatwa kwa makosa ya uzururaji kama inavyofanyika kwa watu wanaojihusisha na biashara ya ngono jijini humo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Ronarl Makona, kwa niaba ya Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, wabunge hao wanatakiwa kuripoti kwa hiari yao Kituo Kikuu cha Polisi jijini.

"Kwa wale ambao bado wapo jijini Dar es Salaam, wanatakiwa kwa hiari yao kuripoti Ofisi ya Upelelezi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kwa mahojiano," jeshi hilo liliagiza.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na agizo la Makonda ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wabunge wote ambao hawajatii agizo hilo, wanapaswa kuripoti kwa jeshi hilo ili wahojiwe.

Juzi, Makonda alisema mbunge anayepaswa kubaki Dar es Salaam ni yule mwenye kibali kutoka kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai.

"Asiyekuwa na kibali huyo ni mzururaji kama wazururaji wengine, kipindi hiki ni hatari na tunawataka watu wanaotoka nyumbani ni wale wanaofanya kazi, hatujaalika wazururaji kutoka mkoani kuja kuzurura.

"Inawezekana wakahatarisha zaidi maisha ya wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwaambukiza corona," alisema. Makonda alisema kipindi hiki ni muhimu katika Bunge cha kujadili bajeti ya serikali ili wananchi wapate mahitaji yao.

"(Wananchi) wanahitaji barabara, wanahitaji maji, umeme, wanayo mahitaji mengi ndiyo maana waliwachagua muende Dodoma kupigania mahitaji yao na wala siyo kuzurura.

"Saa 24 baada ya hapo tusilaumiane, tutakukamata kama tunavyokamata machangudoa wanaozurura usiku," alisema.

Wakati hali ikiwa hivyo jijini Dar es Salaam, bungeni jijini Dodoma jana, wabunge wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), waliwataka wenzao kurejea bungeni ili kuchapa kazi huku wakibainisha kuwa hawana ugomvi na viongozi wa chama hicho.

Wabunge hao ni wa Moshi Mjini, Jaffapry Michael na wa Kilombero, Peter Lijualikali, ambao wao na wengine tisa wameendelea kuhudhuria vikao vya Bunge licha ya agizo la chama kuwataka wasihudhurie bungeni na wajitenge kwa siku 14.

Juzi, Spika Ndugai aliwasihi wabunge hao kurejea na iwapo hawatafanya hivyo warejeshe Sh. milioni 110.1 walizolipwa kwa ajili ya kujikimu na kama watarudi baada ya siku 14, lazima wapeleke uthibitisho wa daktari kuwa wamepima corona.

***Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Salome Kitomari (DODOMA)**

# DC afariki dunia

**Na Enock Charles**

MKUU wa Wilaya ya Nyang'hwale, Hamim Gwiyama, amefariki dunia katika Hospitali ya Rufani Bugando alikokuwa akipatiwa matibabu baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Katika taarifa iliyotolewa kwa umma jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, ilibainisha kuwa kifo hicho kilitokea jana saa tano asubuhi katika hospitali hiyo iliyoko jijini Mwanza.

Katika taarifa yake hiyo, Waziri Jafo alieleza wasifu wa marehemu, akisema aliteuliwa na Rais Dk. John Magufuli Juni 26, 2016 na kuwa kabla ya uteuzi huo, aliwahi kufanya kazi sehemu mbalimbali nchini.

Alisema taratibu zingine za mazishi zitaendelea kutolewa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkoa wa Geita.

Kifo cha Gwiyama kimetokea ikiwa ni siku chache baada ya Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evod Mmanda, kufariki dunia usiku wa kuamkia Aprili 27 mwaka huu.



Mfanyakazi wa Benki ya BOA, Nahami Mwaipyana, akiwa chini wa ulinzi wa askari Polisi, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana, akikabiliwa na mashtaka manane ikiwamo wizi na kutakatisha fedha zaidi ya Sh. milioni 85 mali ya mwajiri wake. **PICH: MIRAJI MSALA**.

twiga cement

HEIDELBERGCEMENTGroup

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**

**TAARIFA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka 2020 wa Wanahisa utafanyika kwa njia ya mtandao. TPC PLC inajali sana usalama kuliko mambo mengine yote. Uamuzi wa kuufanya huu mkutano kwa njia ya mtandao ili kupunguza mikusanyiko ya watu na kulinda afya pamoja na usalama wa wanahisa wetu, wafanyikazi wetu, wakurugenzi wetu na washikadau wengine dhidi ya maambukizo ya virusi vya Corona.

**Tarehe na Muda: Alhamisi, tarehe 28 Mei, 2020, saa nne asubuhi**
**Uendeshaji Mkutano: Kwa njia ya mtandao, wenyeji wakiwa Chorus Call Africa**

**DONDOO**

1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu asome taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 27 uliofanyika tarehe 7 June 2019.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2019.
4. Kupokea, kujadili na kama litaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2019.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2020.
6. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

**Kwa Niaba ya Bodi**
**Tarehe: 8 Mei, 2020**

**Alfonso Velez**
**Mkurugenzi Mtendaji**

157351

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com).
2. Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwa CAD Securities Limited (kupitia anwani ya Barua Pepe: judith@cadsecurities.com au neemak@cadsecurities.com au utume picha ya fomu iliyojazwa kupitia Whatsapp [namba: +255 777 787 845]) angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
3. Wanahisa wanaombwa kuwasiliana na CAD Securities Limited kupitia barua pepe tajwa au namba ya Whatsapp tajwa, ili kupata maelekezo zaidi kuhusu jinsi ya kushiriki kwenye Mkutano Mkuu.
4. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com).

# Waziri: Haya ndiyo mambo 7 yanayomwangamiza mkulima

## Afichua siri Morogoro kupindua 'The Big Four' uzalishaji nafaka

**Na Sanula Athanas,**

ALIYEKUWA DODOMA

**JANA Waziri Japhet Hasunga aliweka wazi mambo makuu anayoamini yanakifanya kilimo kichechemee; wakurugenzi wa halmashauri kumpoka mabwana shamba kwa kuwapangia majukumu tofauti na ajira yao, naye akaanika mikakati aliyosuka 'kujibu mapigo' kwa kufikisha ufanisi wa kilimo kileleni.**

**Leo, ana orodha nyingine ya mambo yanayomwangusha mkulima na ufafanuzi uliojitosheleza, pamoja na siri ya Mkoa wa Morogoro kuibuka kinara anayezipiku 'The Big Four' kwa maana ya mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya na Rukwa katika uzalishaji nafaka nchini, hususan mahindi. Endelea kufaidika na simulizi zake:**

**SWALI: Nini shida kuu ya mkulima wako na unaikabili vipi? Mradi wa REA unamsaidiaje mkulima wako?**

**HASUNGA:** Matatizo makubwa yanayomkabili mkulima kwa sasa yako matatu, manne au zaidi ya hapo. Tatizo la kwanza ni upatikanaji wa masoko ya uhakika, ili aweze kujua kwamba aende kulima na akilima atakwenda kuuza sehemu fulani. Hili ni tatizo kubwa.

Tatizo la pili, ni maarifa na tija kuwa ndogo. Wengi wanakwenda kulima bila kuzingatia kilimo cha kisasa, hawazingatii upatikanaji wa mbegu zinazostahili, hawazingatii viuatilifu na mbegu zinazohitajika.

Kwa hiyo, matokeo yake tija imekuwa ni kidogo sana kuliko hali halisi ya ardhi tuliyonayo na uzalishaji ambao uliokuwa unahitajika kama wangelima kwa utaalamu. Imekuwa ni dosari kubwa.

Eneo la tatu ambalo mkulima linamkabili sana ni namna ya kupata mikopo na ufadhili wa kuwekeza kwenye kilimo. Kumekuwa na tatizo kubwa sana kwa sababu mkulima analima mara moja kwa mwaka, akipata hizo fedha, kuzitunza mpaka mwakani zimsaidie kwa kilimo inakuwa ni mtihani.

Na kwa bahati mbaya, mifumo ya kibenki na mifumo ambayo tunakuwa nayo, haimwezeshi kwenda kukopa sehemu fulani, akakopa sehemu fulani, akaenda kuwekeza tena, akaendelea na kilimo kama kawaida.

Kwa hiyo, 'financing' (uwezesho wa kifedha) imekuwa ni tatizo kubwa linalowakumba na kuwaathiri sana wakulima wetu.

Jambo la nne ni kuwa uwezo wa viwanda vya kuongeza thamani, ili badala ya kwamba kile anachokizalisha akiuze kama kilivyo, awe anakiongeza thamani kidogo kusudi aingize fedha nyingi. Hii nayo imekuwa dosari.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (mwenye fulana nyeupe) akiwa na wenyeji wake, wakulima katika shamba la mahindi wakati alipozindua msimu wa kilimo kitaifa wa sasa, mnamo Novemba 22 mwaka jana huko Vwawa, Mbozi mkoani Songwe, moja ya maeneo vinara kitaifa katika uzalishaji wa zao hilo. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**.

Uwezo wa wakulima kuongeza thamani ya mazao yao, kuzalisha na kupanga kwa madaraja, bado ni tatizo nchini. Yaani 'grading system' ya kwetu unakuta mtu amezalisha nyanya ndogo, kubwa, mbaya, zilizoharibika, zote zinawekwa kwa pamoja.

Akiwa na uwezo wa kuzichambua na akazipanga kwenye madaraja, ingemwezesha kupata hela nzuri zaidi kuliko mfumo ambao upo sasa hivi. Hizi ni dosari ambazo zipo.

Lingine ni maarifa madogo na kutopatikana kwa utaalamu wa kutosha kutoka kwa maofisa ugani. Ushirikiano wa wakulima na maofisa ugani bado ni mdogo sana, kwa sababu maofisa ugani wengi wamekuwa hawathamini wakulima.

Maofisa ugani hawaendi kwa wakulima, wanataka wakulima ndiyo wawatafute na hata wakiwatafuta au kuwafuata, wamekuwa hawatoi huduma inayotakiwa.

Lakini, nina imani kabisa, kwa kadri siku zinavyozidi kwenda, watu wanahamasika. Tunataka sasa wakulima wetu wawe watu waliosoma, walioelimika, wenye uwezo wa kuchanganua mambo. Hii itasaidia sana.

> "Kuhusu REA, hakuna ubishi imewasaidia kwa kiwango kikubwa wakulima kwa sababu sasa hivi wana uwezo wa kukausha mazao hata kama mvua kubwa ikinyesha.

Tatizo lingine kubwa kwa wakulima ni uwezo wa kutunza kumbukumbu za gharama za uzalishaji, hawana! Asilimia 95 ya wakulima wetu hawana uwezo wa kutunza kumbukumbu. Kwa hiyo, hawajui kuwa wanalima kilimo cha faida au cha hasara.

Kwa kulitambua hilo, tunataka waondokane na kilimo cha kujikimu, waende kwenye kilimo cha kibiashara. Ninaposema waende kwenye kilimo cha kibiashara maana yake hata kumbukumbu watunze; wajue nimegharamika kiasi fulani, nimeweka hiki kiasi fulani.

Hata nguvu yake ile aithamanishe, aiweke kwenye thamani ili tujue kwamba gharama za uzalishaji ni kiasi gani. Je, alichokiwekeza, amepata faida au hasara? Hiyo inakuwa tatizo kubwa ambalo linawakumba sana wakulima wetu nchini. Hayo ndiyo mambo ambayo yapo kwa upande wa mkulima.

La mwisho, ni teknolojia duni. Hii nayo imekuwa ikimwathiri sana mkulima. Imemfanya asifikie malengo anayoyatarajia. Wengi wanatumia jembe la mkono, sisi tunataka tutumie trekta, tutumie utaalamu wa kisasa katika kulima, lakini ni wachache wenye uwezo wa kumudu hivyo vitu.

Kwa hiyo, wakulima wengi bado wanatumie jembe la mkono. Hata wale wanaotumia jembe la ng'ombe, bado wako kwenye kilimo cha zamani. Sasa tuna kilimo cha kisasa ambacho hakitakiwi ulime ardhi, tunakiita 'smart agriculture'. Haitakiwi ulime ardhi, usiharibu mazingira. Sasa, wengi hawajaweza kumudu.

Kuhusu REA, hakuna ubishi imewasaidia kwa kiwango kikubwa wakulima kwa sababu sasa hivi wana uwezo wa kukausha mazao hata kama mvua kubwa ikinyesha.

Sasa, wakulima wetu vijijini wanao uwezo wa kukausha mazao kwa kutumia umeme walionao. Kutokana na umeme kuwafikia, hata uhifadhi wa chakula utakuwa mzuri.

Wanaweza kutumia teknolojia ya kisasa kuhifadhi chakula. Mkulima sasa anaweza kukausha mazao yake vizuri, na umeme huu umetusaidia kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kufungasha yale mazao na kuongeza thamani.

Sasa unakuta wengine wanatengeneza hiki, wengine wanatengeneza hiki, wanaweza hata kufungasha chipsi za kisasa na hata kwenye muhogo kwa mfano, unaweza kukausha. Kwa hiyo, umeme huu kwa kweli una mambo mengi.

**SWALI: Miaka ya 1980 ilikuwapo mikoa minne mabingwa wa kuzalisha nafaka nchini hasa mahindi. Leo ni ipi? Kama kuna mabadiliko, kwanini? Morogoro sasa unatikisa, imeibukaje?**

**HASUNGA:** Bahati mbaya Morogoro mwaka huu wameathirika sana kutokana na mafuriko, mvua imezidi sana wameathirika, lakini ninataka nikwambie tu kwamba Morogoro wana ardhi nzuri sana. Wana mabonde mazuri yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Pia, sasa hivi mwamko wa watu kuwekeza kwenye kilimo ni mkubwa sana, watu wameamka sana! Kwa hiyo, hili limefanya mikoa inayofanya vizuri kwenye kilimo iongezeke zaidi.

Kwa mwaka jana, mikoa ambayo ilionekana ina uzalishaji mkubwa na wa kutosha ilikuwa kumi na mmoja (11). Sasa si mikoa mitano wala minne, wala si mikoa saba.

Zamani tulikuwa na mikoa minne (Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Iringa). Sasa baadhi ya hiyo mikoa imegawanywa. Mbeya imekuwa mikoa miwili (Mbeya na Songwe), Rukwa nako kumekuwa na Rukwa na Katavi, Iringa imezaa Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo, mikoa hiyo vinara wa uzalishaji chakula imekuwa saba.

Kwa hiyo, mikoa iliyokuwapo awali imeungana na mikoa ambayo hapo katikati imeongezeka katika uzalishaji. Kigoma, Morogoro nayo imeongezeka katika uzalishaji.

Sasa, mikoa mikubwa yenye uzalishaji wa kutosha kwa upande wa chakula, ni zaidi ya 11 na inafanya vizuri. Tunatarajia mwaka huu tutapata mikoa mingi zaidi yenye uzalishaji mkubwa kwa sababu watu wamehamasika sana karibu nchi nzima. Na bahati nzuri mvua imenyesha nchi nzima, uzalishaji utakuwa mkubwa sana.

***JE, KILIMO KWANZA KIPO AU HAKIPO? USIKOSE KESHO MAJIBU YA KINA TOKA KWA WAZIRI.**

## Ofisa Takukuru `feki' mbaroni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (Takukuru), inamshikilia Simon Jumbe, kwa kosa la kujifanya ofisa wa Takukuru na kuwatapeli watu Sh. milioni 2.5 kwa madai ya kuwatafutia kazi katika taasisi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema mtuhumiwa huyo aliyejifanya mfanyakazi wa Takukuru, alikuwa akichukua fedha hizo akiwadanganya watu za kwenda kununulia sare za kazi, kufungua akaunti kwa ajili ya mshahara pamoja na nauli ya kwenda kuapishwa jijini Dar es Salaam, baada ya kupata kazi hiyo.

"Huyu aliwaambia kwamba Takukuru imetoa nafasi saba za kazi, tatu tayari zimepata watu bado nne hivyo wampe kiasi cha fedha ndipo awasaidie kupata," alisema.

Alisema awali aliomba Sh. 350,000 ili amsaidie dereva kupata leseni ya daraja C, kitendo ambacho ni cha udanganyifu.

Alisema walifanya uchunguzi na kubaini tapeli huyo amekuwa akifanya mchezo huo kwa kutapeli Sh. milioni 2.5 kutoka kwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) ili amsaidie kupata ajira kama mkurugenzi msaidizi wa Takukuru.

Kadhalika, Taasisi hiyo imewafikisha mahakamani Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Muungano, Wilaya ya Chamwino, Chizenga Masagasi (56) na Salehe Chagulula (45), ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Muungano kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 70,000.

Washitakiwa wote walifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, kwa madai ya kupokea rushwa hiyo ili wasaidie kuhamisha malalamiko la mtoa taarifa kwenda polisi kwa hatua za kisheria.

Alisema watu hao wametiwa hatiani baada ya Takukuru kupata taarifa na kufanya uchunguzi kisha kuwakamata wakiwa wamepokea kiasi hicho cha fedha.

Kibwengo, alisema pia wamemkamata Mwenyekiti wa Kitongoji cha Iyopo, Wilaya ya Chamwino kwa kosa la kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. 25,000 kutoka kwa mtoa taarifa ili aitishe baraza la viongozi kusikiliza shauri lake.

Alisema hata hivyo, mtuhumiwa huyo hakufanikiwa baada ya kujikuta yupo mikononi mwa Takukuru.

Taasisi hiyo pia imefanikiwa kuokoa Sh. milion 194 za vyama vya ushirika kutoka kwa viongozi 41 wa vyama sita ambao walikuwa wanaidaiwa kwa muda mrefu.

Kibwengo alisema fedha hizo wanatarajia kuzikabidhi kwa Mrajis wa vyama ili ziweze kurejeshwa kwa wahusika wakati wowote kuanzia sasa.

Katika hatua nyingine, Takukuru imebaini matumizi mabaya ya fedha za ujenzi wa ofisi ya mtendaji wa kata ya Mnadani kwamba vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya Sh. milion 5.2 havikufika.

Taasisi hiyo pia imekionya Chama cha Walimu (CWT) kujiepusha na vitendo vya rushwa katika uchaguzi unaoendelea wa kupata viongozi.

# Rugemalira agonga mwamba

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imetupilia mbali hoja za washtakiwa mfanyabiashara James Rugemalira na wenzake za kutaka kuondolewa mashtaka kutokana na hati ya mashtaka hayo kuwa na upungufu wa kisheria na waachiwe huru.

Kadhalika, mahakama hiyo imesema haina mamlaka ya kumuamuru Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) au kuwaachia huru washtakiwa kwa sababu kesi yao inasikilizwa na Mahakama Kuu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili.

Februari 29, mwaka huu Rugemalira aliwasilisha hoja ya kumtaka DPP atoe kibali cha kumwachia huru na kwamba asipofanya hivyo mahakama hiyo imwondolee mashtaka yanayomkabili.

Mshtakiwa wa tatu, Joseph Makandege, aliwasilisha hoja zake Machi 26, mwaka huu akidai hati ya mashtaka ina upungufu wa kisheria.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikiliza uamuzi mdogo wa mapingamizi ya awali ya mshtakiwa wa kwanza na wa tatu.

Hakimu Shaidi alisema mahakama yake haina mamlaka ya kutekeleza hoja za washtakiwa kupitia mapingamizi yao ya awali bali wajibu wake ni kuitaja na kusoma maelezo ya mashahidi ikiwa upelelezi umekamilika na DPP kutoa kibali kwa Mahakama Kuu kuendelea kusikiliza kesi hiyo.

"Mahakama yangu imepitia hoja za mapingamizi ya washtakiwa na yote mnayoyalalamikia haina mamlaka ya kuyafanyia kazi wala kutoa amri hivyo kama mnaona kuna mambo hamridhiki nayo naomba mpeleke hoja zenu Mahakama Kuu," alisema Hakimu Shaidi.

Mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni, Harbinder Seth, ambaye aliiomba mahakama hiyo isaidie kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo kwa kuwa umechukua muda mrefu kuanza kusikilizwa mbali na uamuzi alioufanya mwaka jana wa kuandika barua ya kukiri makosa na kuomba makubaliano na DPP bila kupata majibu.

Akijibu hoja ya Seth, hakimu Shaidi alisema hakuna mahakama inapenda kuchelewesha kesi na kuongeza kuwa kama angekuwa na mamlaka angeshaifuta.

Kuhusu barua aliyoiandika kwa DPP hakimu alisema kuwa utaratibu huo wa kisheria ni kati ya ofisi ya DPP na mshtakiwa, hivyo mahakama haihusiki kwa chochote bali inasubiri taarifa tu kutoka kwa pande hizo mbili.

Baada ya uamuzi huo kutolewa mshtakiwa Rugemalira alikubaliana na uamuzi wa kwenda Mahakama Kuu na kuomba apatiwe nakala uamuzi huo mdogo.

Hakimu alisema kesi hiyo ilitajwa Mei 21, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Washtakiwa Seth na Rugemalira kwa pamoja na Joseph Makandege, wanakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Rugemalira na Seth walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Juni 19, 2017.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Azza Hilali (kushoto), akikabidhi kompyuta kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Shinyanga, Shambuo Katambi, kwa ajili ya matumizi ya kazi za chama, katika hafla iliyofanyika jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bavicha yamjibu Makonda kukamata wabunge Chadema

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Bavicha), limemjia juu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kutokana na kauli yake ya kutangaza kuwakamata wabunge walio katika mkoa wake ambao hawashiriki vikao vya Bunge vinavyoendelea jijini Dodoma.

Kauli hiyo ya Bavicha imekuja ikiwa ni siku moja baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kutangaza kauli ya kuwakamata wabunge ndani ya saa 24, ambao hawashiriki katika vikao vya Bunge na kuonekana katika mkoa wake.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bavicha, Apollo Boniface, ilisema ni vyema Makonda akaacha kukurupuka na kuzingatia kutimiza majukumu yanayomhusu.

"Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kupitia vyombo vya habari, tumemsikia akitoa saa 24 kwa wabunge waliopo Dar es Salaam kurejea Dodoma na kusisitiza kuwa mbunge anayetakiwa kuwa katika mkoa huo ni yule ambaye ana kibali cha Spika, pia akawafananisha wasiokuwa na kibali hicho ni sawa na wazururaji, hivyo atawakamata kama wanavyowakamata machangudoa usiku," alisema Boniface.

"Baraza tunamtaka Makonda kuheshimu na kufuata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo imetoa uhuru kwa kila Mtanzania kwenda popote bila kushurutishwa au kufukuzwa, katika ibara ya 17(1) inasema kila raia anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia."

"Pia inasema kila raia ana haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano. Ibara ya 15 (1) imesisitiza uhuru wa kila mtu na anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru."

Boniface alisema kwamba kama ilivyoelekezwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, wabunge wao wako karantini.

"Wabunge wetu wapo karantini kama walivyoelekezwa na chama tangu Mei Mosi, mwaka huu. Haki hii tuliyopewa na Katiba itakuwa mwongozo kwetu kama Baraza na siyo kauli za baadhi ya viongozi wa serikali, tutailinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwalinda viongozi wa chama pamoja na wabunge wetu dhidi ya aina yoyote ya udhalilishaji na ukandamizaji, tutakuwa mstari wa mbele kusimamia uamuzi wa chama na tunawataka viongozi wa kiserikali kuheshimu na kufuata uamuzi wa chama chetu," alisema Boniface.

"Baraza tunamtaka Makonda asitupime nguvu yetu vijana, aache kukurupuka, atimize majukumu yake kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi yetu."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kurejeshea maji waliokatiwa hatua muhimu vita ya corona

WAKATI huu ambao dunia inaendelea kukabiliana na janga la ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, moja ya vitu muhimu vinavyohimizwa na wataalamu wa afya, ni matumizi ya maji tiririka kwa ajili ya kunawa mikono na sehemu zingine za mwili ambazo zinaweza kupata maambukizo ya virusi.

Pamoja na kuhimizwa matumizi ya maji tiririka, kuna changamoto kwamba si watu wote wanapata majisafi ya kunawa kama sehemu ya kujikinga, kutokana na baadhi kusitishiwa huduma za maji na mamlaka za maji kwa sababu ya madeni ya Ankara.

Kimsingi, hali hiyo inakuwa ni kikwazo dhidi ya kujikinga kwa kila mmoja kunawa mikono kwa kutumia maji tiririka na sabuni, tena wakati huu ambao watu wengi wameitikia ushauri na maelekezo ya wataalamu wa afya na serikali.

Jambo la kutia moyo ni uamuzi uliotangazwa jana na serikali wa kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) kuwarejeshea huduma za maji wateja wote nchini waliokatiwa huduma hiyo kutokana na madeni kwa makubaliano.

Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso, katika uamuzi huo ilifafanua kuwa lengo ni kuwawezesha wananchi wengi kupata huduma hiyo katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa COVID 19.

Aweso alitoa agizo hilo jijini Dodoma alipokutana na kuzungumza mambo mbalimbali na menejimenti ya Ewura, yakiwamo malalamiko ya ankara kubwa za maji zinazotolewa kwa wateja.

Alisema taifa liko katika mapambano na vita dhidi ya corona, hivyo jambo muhimu ni kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu.

Alisema silaha pekee ya kukabiliana na maambukizo ya virusi hivyo ni maji tiririka na kunawa kwa sabuni, serikali imeamua wateja wote waliokatiwa maji warejeshewe kisha Ewura iweke utaratibu mzuri wa kulipa madeni yao.

Alieleza kuwa, zipo mamlaka za maji ambazo ni vinara kwa kuwabambikia na kuwapandishia wananchi bei za maji kiholela, hivyo aliiagiza Ewura kuhakikisha inafikisha ripoti ya mamlaka za aina hiyo wizarani ili kuzichukulia hatua stahiki, kwa kuwa mana wizara ndiyo yenye mamlaka ya mwisho.

Uamuzi huo unastahili kupongezwa kwa kuwa serikali imeona kuwa wenye madeni ya ankara za maji kukosa huduma hiyo kutarudisha nyuma jitihada zinazochukuliwa za wananchi kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Lakini pia, kauli za Naibu Waziri Aweso zinaonyesha kuwa hata serikali imebaini mchezo mchafu unaofanywa na baadhi ya mamlaka za maji nchini kuwabambikia watumiaji wa maji ankara za maji zisizo na uhalisia, hivyo kushindwa kulipa na matokeo yake kukatiwa huduma.

Hatuamini kama kuna mtumiaji wa maji anayeweza kukaidi kulipa Ankara ya maji makusudi, hivyo tunaona ulazima wa Ewura kulichukua suala la ankara kubwa za maji zisizo na uhalisia kama changamoto ya kuifanyia uchunguzi na kuipatia suluhisho la haraka.

Tunachokihisi ni kuwa baada ya serikali ya sasa kuzibana mamlaka za maji kuacha kufanya kazi kwa mazoea ya kutegemea kupewa ruzuku kutoka serikalini, baadhi ya mamlaka zinawabambikia ankara watumiaji ili kupata mapato zaidi ya kujiendesha.

Ni matarajio yetu kuwa Ewura itatekeleza maagizo yote iliyopewa na serikali kama ilivyoahidi haraka iwezekanavyo hususan kurejeshea watumiaji maji huduma na kuweka utaratibu mzuri wa kulipa.

Utaratibu wa kulipa madeni hayo haunabudi kwenda sambamba na wateja kushirikishwa kwa uwazi na mamlaka husika za maji katika suala la ankara ili kuepukana na Ankara zisizo na uhalisia.

Ewura pia izisimamie mamlaka za maji kuhakikisha zinaweka dawa za kutibu maji wakati huu wa tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona. Kwa kufanya haya, ni matarajio yetu kuwa tutakuwa timechukua hatadhari ya kutosha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Uuzaji barakoa kwa mtindo 'sagurasagura' si salama

Na Sabato Kasika

**HII** ndiyo hali halisi iliyopo sasa katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, hasa kwenye vituo vya mabasi vikiwamo vya daladala. Ni hali gani hiyo? Mauzo ya barakoa yanazidi kushamiri.

Utakuta wake kwa waume na makudi ya vijana, wanaranda kila upande wameshikilia lundo la barakoa, wengine wamezipanga kwenye meza kutangaza biashara hiyo inayozidi kupata umaarufu sio katika jiji hili, bali kwingi.

Imekuwa maarufu karibu kila kona, hasa wakati huu ambao nchi inapambana dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona, ambavyo ni tishio kwa dunia.

Barakoa zinauzwa kwa lengo la kuwakinga watu dhidi ya maambukizo ya virusi hivyo wakati wa kuongea, kupiga chafya na kukohoa. Pia, inazuia mate na majimaji kutoka kinywani au puani kuwarukia wengine.

Katika kukabiliana na gonjwa hilo, Watanzania wameelekezwa kutumia vifaa hivyo, kama njia mojawapo ya kuepuka maambukizo na sasa baadhi ya watu wamegeukia biashara ya kushona na kuziuza.

Hali ya sasa katika biashara hiyo, kuna hitaji la elimu ya haraka kwa umma, kwani ikiachwa kiholela kuna hatari ya kuchangia kuenea kwa virusi hivyo, badala ya kupunguza maambukizo, kama inavyokusudiwa.

Mauzo ya barakoa kwa sasa yanafanywa katika mtindo unaofanana sana na uuzaji wa nguo za mitumba, ambazo wateja wake huchagua nguo anayokusudia, anajipima na kisha anafikia uamuzi wa ama kununua au la. Jina la hilo kwa ufupi ni 'sagurasagura'.

Yaani, mteja anafika kwa muuzaji wa barakoa na anachambua hata kufikia kile akipendacho, kwa mtindo uleule wa biashara ya nguo anakisaka akipendacho.

Msingi wa mazingira ya namna hiyo si salama katika kukabiliana na virusi vya corona, kwani yanaweza kuongeza maambukizo kama wauzaji na wateja wao hawatachukua tahadhari zinazotakiwa.

Kwa mtindo huo wa wauzaji kuruhusu wateja kujaribu kuvaa barakoa kabla ya kuzinunua, ni wazi kwamba kuna hatari ya wateja wao kujikuta wakiambukizwa kwa kutojua au wakiwa wanajua.

Mtu anaweza kuwa tayari ameambukizwa na akaenda kujaribu kujipima barakoa, hali inayoweza kuwa chanzo cha kuacha virusi kwa muuzaji na hata wateja wengine.

Tahadhari zilishachukuliwa, ikiwamo kuzuia mikusanyiko mikubwa katika maeneo mbalimbali, kuliko zilizozoeleka katika maeneo kama maeneo ya ibada na sokoni.

Inashauriwa, zama zilizopo siyo za kuuza barakoa wala kununua kwa mtindo wa 'sagurasagura,' kwani inaweza kusababisha maambukizo kuendelea kuwapo nchini.

Hata wauzaji wanaopanga barakoa kwenye meza huku zikipigwa na vumbi huku wateja nao wakishika moja baada ya nyingine, inaweza kuwa na mwendelezo wa kusambaa maambukizo ya maradhi hayo.

Baadhi ya mafundi wa kushona nguo, kwa sasa wamejikita kushona barakoa, kwa sababu ndiyo biashara msimu huu wa corona, lakini wanaozinunua kwa jumla na kwenda kuuza mitaani wawe makini.

Zipo barakoa za kuanzia bei ya Sh. 500 na kuendelea, zinazouzwa maeneo mbalimbali na kwenye mikusanyiko ya watu wengi vikiwamo vituo vya daladala, lakini tatizo ni baadhi ya wauzaji na wateja kutozingatia afya.

Kila mmoja atambue kuwa kuuza barakoa kwa mtindo wa 'sagurasagura' si salama kabisa, kinachotakiwa ni pande zote mbili kuchukua tahadhari katika biashara hiyo inayoendelea kupata umaarufu.

Pamoja na hayo, ni vyema pia mamlaka husika kutoa malekezo yatakayosaidia kuwafanya wauza barakoa na wateja wao kutambua kuwa uuzaji na ununuaji wa vifaa hivyo haufanani na biashara ya nguo za mitumba.

Hapa umakini mkubwa unahitajika kwa ajili ya usalama wa wauzaji na wateja wao hasa kutokana na ukweli mdomo, macho pia ni viungo vinavyotajwa kuwa na uwezekano wa kupitisha virusi hivyo.

Ni bahati mbaya baadhi ya wateja wamekuwa wakichagua barakoa na kujaribu kuzivaa na kuacha, kwa lengo la kutaka kupata zile zinazowafaa, lakini inasemekana mtindo huo si salama kiafya.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akionyesha baadhi ya silaha na mikasi walizozikuta kwenye gari namba T 7777 DSJ aina ya Toyota Crown, baada ya kuwakamata majambazi wanne akiwamo na mganga wa kienyeji toka wilayani Magu mkoani Mwanza, wakati wakitokea Dar es Salaam kwenda Arusha kufanya uhalifu. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**.

# Polisi yazima tukio la ujambazi, wanne mbaroni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, limefanikiwa kuzima jaribio la uhalifu kwa kuwakamata watuhumiwa wa ujambazi wanne akiwamo mganga wa kienyeji wakiwa na silaha za moto.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Mei 6, majira ya saa 4:00 usiku eneo la daraja la Mto Nduruma, Kata ya Baraa, Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Steve Godfrey (32), mfanyabiashara na mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, Yunusi Hamed (37), mfanyabiashara na mkazi wa Korogwe, mkoani Tanga.

Wengine ni Said Hamisi (38), mfanyabiashara na mkazi wa Dar es Salaam na mganga wa kienyeji Msafiri Yohana (22), mkazi wa Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza.

Kamanda Shana alisema jeshi hilo lilipata taarifa za siri na kuiweka mtego wao uliofanikiwa kuwatia nguvuni.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wakitokea Dar es Salaam kwenda Arusha kwa kutumia gari aina ya Toyota Crown lenye namba za usajili T.777 DSJ.

"Nia ya majambazi haya ilikuwa kutaka kufanya uhalifu hapa jijini Arusha, lakini kikosi kazi kabambe kiliweka mtego eneo la Mto Nduruma na ulipofika muda tuliambiwa, tuliona gari hili linapita na askari wangu walipojaribu kulisimamisha waliongeza mwendo mkali na askari wakamua kufyatua risasi kupiga tairi za gari hilo na likakosa mwelekeo likagonga kingo za mto huo," alisema.

Alisema gari hilo lilisimama baada ya kugonga kingo, huku Yohana ambaye ni mganga wa kienyeji akitoa mikono yake nje ya madirisha ya gari hilo na kuonyesha chupa yenye dawa hali iliyolazimisha askari kumjeruhi kwa risaisi mikono hiyo, huku wenzake wakishuka na kunyanyua mikono kama ishara ya kujisalimisha.

"Tulipowapekua ndani ya gari tukakuta shotgun moja, bastola, risasi nne za bunduki ya shotgun, risasi nane za bastola zilizokuwa kwenye magazine, mikasi mitatu ya kukatia vyuma, nondo mbili na gundi na madawa mbalimbali ya mitishamba," alisema.

Alisema baada ya kukamata vitu hivyo na kuwahoji, watuhumiwa hao walikiri kuja Arusha kufanya uhalifu kwa kusaidiana na mganga huyo ili wasionekane.

Pia, walimtaja mwenyeji wao ambaye aliwaita waje wafanye uhalifu kwa pamoja mkoani hapo.

"Alipokua anaonyesha kile kichupa askari wetu waliamini askari watasinzia na kutowaona maana ndio wanavyotumia huko walikofanya uhalifu, Morogoro, Tanga, Dar es Salaam na Mwanza," Kamanda alisema.

Aliwaonya watu wote wenye nia ya kufanya uhalifu mkoani Arusha kuacha kwa sababu hawatafanikiwa na hata mwenyeji wao watamkamata wakati wowote. "Mtaingia salama lakini hamtatoka salama, kwa sababu jeshi langu limejipanga vizuri na watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani wakati wowote," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliwapongeza askari hao na kuomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, SimbaChawene na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro, kuwaangalia askari na kamanda wao Shana waliofanikisha kukamatwa kwa majambazi hayo na silaha.

# Uhamiaji yakamata raia kigeni 17 kuingia nchini

**Na Edina Alex,** SINGIDA

IDARA ya Uhamiaji Mkoa wa Singida imewakamata wahamiaji haramu 17 kwa madai ya kuingia nchini bila kufuata taratibu.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa jana, Kamanda wa Uhamiaji Mkoa wa Singida, Safina Muhindi, alisema kuanzia kipindi cha Januari hadi Aprili, mwaka huu wamewakamata raia 17 waliotoka mataifa mbalimbali walioingia nchini bila kufuata taratibu za Uhamiaji.

Alisema raia hao waliingia mkoani hapo walikutwa kwenye maeneo ya migodi na soko la kimataifa la vitunguu na kubainika kuwa raia hao kwenye mabano na nchi zao kuwa China (3), India (3), Yemen (2), Ethiopia (2), Burundi (1), Kenya (2), Congo (1), Rwanda (1) na Somalia (2).

"Wahamiaji hawa haramu tuliwakamata wakiwa soko la kimataifa la vitunguu hapa Manispaa ya Singida na kwenye mgodi wa Sekenke, wilayani Iramba kupitia doria zetu ambao walikuwa wakiendelea na shughuli kwenye maeneo hayo huku wengine wakidanganya na kujitambulisha kuwa ni raia wa Tanzania," alisema Muhindi. Alisema baada ya uchunguzi wa kina wahamiaji hao haramu walibainika kuwa wameingia kimakosa nchini na wamechukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikiwamo kulipa kibali maalumu kama adhabu.

"Hiki ni kibali maalumu ambacho hutolewa kwa wageni kama adhabu ambao walichelewa kuhuisha vibali vyao kwa muda kwa hiyo hii ni miongoni mwa adhabu tulizozitoa kwa wahamiaji hao," alisema Muhindi.

Aliwataka Watanzania kushirikiana kutoa taarifa wanapomuona ama kumtilia shaka raia wa kigeni ili kuzuia nchi isitumike kama sehemu ya kichaka cha wahamiaji haramu huku akiwataka kufuata sheria na taratibu zote za kiuhamiaji.

# TPSF yaahidi kuendeleza ubunifu vita dhidi corona

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI YA Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imelihakikishia taifa kwamba wanachama wake wataendelea kwa nguvu zoke kukomaza ubunifu katika kupambana na ugonjwa wa corona kutokana na serikali kuruhusu uzalishaji uendelee.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema taasisi yake itaendelea kuunga mkono serikali katika jitihada yake ya kupambana na janga la corona.

"Tunaendelea kuipongeza Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla kwa jitihada zinaoendelea kuchukuliwa. TPSF kwa kushirikiana na wadau wetu tutakuwa bega kwa bega katika kuunga mkono jitihada hizo mpaka pale tutakapohakikisha kasi ya maambukizo inapungua na kupotea kabisa," alisema Ngalula.

Jumatatu, taasisi hiyo ilitoa fedha na vifaa vya kupambana na corona vinavyokadiriwa kuwa na thamani ya Sh. bilioni 2.1.

Ngalula aliishukuru serikali kwa kuruhusu kazi ziendelee katika maeneo yote ya uchumi wa taifa badala ya kuiga hatua za nchi za kigeni ikiwamo kuwafungia ndani wananchi kama hatua ya kujikinga na kuenea kwa maambukizo.

"Kutofunga shughuli za uchumi kumechochea ubunifu kwa wadau wa sekta binafsi. Hivi sasa wamejikita katika uzalishaji wa vifaa vya kujikinga na maambukizo ya corona, ikiwamo barakoa, sanitaiza, ndoo na matanki ya kuimarisha tabia ya watu kunawa mikono.

"Ubunifu wa aina hii umelinda ajira za Watanzania na kuimarisha uchumi wa nchi katika kipindi hiki cha janga," alieleza.

Alisema TPSF imepokea wito chanya wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wa kuwataka wanachama wa taasisi hiyo kutengeneza kila kinachowezekana kuwakinga wananchi na virusi vya corona, vikiwamo vifaa vya kinga na sanitaiza.

Waziri Mwalimu alitoa wito huo Jumatatu jijini Dar es Salaam, wakati akipokea mchango wa TPSF wa fedha na vifaa vya kupambana na corona. Kampuni nane zilitoa vitu mbalimbali kuwasaidia Watanzania kujikinga na maambukizo hayo.



Kamanda wa Polisi mkoa wa Songwe, George Kyando, akikagua maboksi 196 ya vipodozi vyenye viambata vya sumu vilivyokamatwa kwenye mpaka wa Tanzania na Zambia, katika Kata ya Chapwa, Tarafa ya Tunduma, mkoani Songwe. **PICHA: MANUEL KAMINYOGE**

# Vifo vya corona kuchunguzwa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

VITUO vya kutolea huduma za afya nchini, vimetakiwa kufanya uchunguzi wa kifo chochote kitakachotokana na ugonjwa wa corona ili kubaini kama mgonjwa alihudumiwa ipasavyo kabla ya kifo kutokea.

Agizo hilo limetolewa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, jijini Mwanza, baada ya kuagana na uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa – Bugando alipokuwa akifanya kazi awali kama Mkurugenzi Mtendaji kabla ya kuteuliwa na Rais John Magufuli kuwa Mganga Mkuu wa Serikali.

"Kwakweli tusingependa kuona mgonjwa anafariki kwa sababu zisizo na msingi, naagiza hospitali zote zenye kamati ya uchunguzi (Clinical Audit) kufanya uchunguzi wa vifo vinavyohusiana au kutokana na corona ili kuona kama kulikuwa na tatizo lolote katika kumpokea mgonjwa au katika kumhudumia," alisema Prof. Makubi.

Aliwataka wananchi kuelewa kuwa sio kila kifo kinachotokea hivi sasa kinasababishwa na ugonjwa wa corona kwa kuwa yapo magonjwa mengine pia ambayo yanashamblia binadamu.

"Siyo kweli kwamba mgonjwa akiwa na presha, kisukari, figo au kansa akifariki iwe imesababishwa na corona, tuendelee kuwahudumia wananchi, kuepusha vifo vinavyoweza kuwa na uhusiano wa corona," alisema.

Pia, ametoa rai kwa vituo vya afya kuwapokea wagonjwa wote na kuwapatia matibabu bila ya kuwabagua kuwa na dalili za corona.

"Serikali inapenda kuona wagonjwa wa corona wanapokelewa na kupata matibabu, tuendelee kuwapokea na kuwahudumia huku tukichukua tahadhari ya maambukizo."

"Watumishi wa afya wasiwe na ubaguzi wa kuchagua wagonjwa wa kuwahudumia au mpaka apimwe kipimo cha Covid-19 ndio ahudumiwe, tuwapokee wote, lakini wakati huo tukichukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa."

Katika hatua nyingine, Prof. Makubi alisema serikali inaendelea kusambaza vifaa kinga kwa ajili ya kuwawezesha watoa huduma kujikinga na ugonjwa huo wakati wakitoa huduma.

"Serikali imeanza kugawa vifaa kinga kama vile PPE, masks pia sanitizer kwa ajili ya vituo vyote vya afya Tanzania, kwahiyo pasiwapo kisingizio chochote cha kushindwa kumhudumia mgonjwa wa corona kwa sababu ya vifaa kinga."

# Ndugai awataka wabunge wa Chadema kurejea

**Na Salome Kitomari**, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amerudia agizo lake kwa wabunge wa Chadema, akiwataka kurejea bungeni, vinginevyo hawatapewa mshahara wa mwezi wa tano.

Akizungumza baada ya kupitishwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, alisema taarifa za madeni ya wabunge zimeshaletwa na amewaelekeza watumishi wa Bunge kuwafikishia kwa maandishi.

"Bado natafakari mtu aliye mtoro kwa wiki mbili kazini kwake halipwi mshahara bado sifikirii kwenda huko, lakini kwa mtu wa aina hiyo hata serikalini huwa halipwi mshahara, hawa hawastahili kulipwa mshahara wa mwezi wa tano, hivyo wajue wakiendelea kugoma hawatapata na waeleze kwanini wanautaka mshahara wakati hawajafanya kazi," alisema.

Alisema Bunge limepokea taarifa ya bakaa ya mikopo ya wabunge wote kutoka taasisi ambao itatumika katika kukokotoa na kulipa mafao ya hitimisho la ubunge," alisema.

"Nawaelekeza wahasibu watoe barua kwa utaratibu wa kupewa kwa mkono na kusaini kuwa wamepokea kwa maandishi, na si kutumia vishikwambi (Tablets) wabunge waliopo na wasiokuwapo wakae huko ili wakose taarifa na atashangaa kitakachoendelea," alisema na kuongeza:

"Mwisho wa mwezi huu kuna kazi (ukokotoaji) inaendelea, basi watashangaa...wapo kwenye mtihani mkubwa wa kumtii huyo jamaa yao (Freeman Mbowe) au kurudi bungeni kuendelea na kazi zao."

"Mbunge anapochangia au anapofanyakazi zake anapaswa kuangalia taratibu za nchi, kanuni za kibunge, atazame jambo linaloendelea lina maslahi gani kitaifa.. lazima aangalie wananchi waliomtuma na kupata nafasi ya kuchangia, na chama kilichomtuma na mbunge mwenyewe kujiuliza juu ya barua ya Freeman Mbowe," alisema.

# Viongozi Waislamu washauri waumini kukaa nyumbani

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa dini ya Kiislamu wamewashauri waumini wao kuzingatia ushauri wa kukaa nyumbani na kusali wakati huu wa janga la corona kwa kuwa hata Kurani inasema jukumu kubwa walilonalo ni kulinda maisha yao.

Hayo yalisema jana katika mkutano wa pamoja uliohusisha baadhi ya viongozi wa dini hiyo, Afrika na India pamoja na taasisi za dini za kimataifa ulioandaliwa na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (Unicef) Tanzania na Unicef Africa.

Shirika hilo lilishirikiana na Baraza la United Religions Initiative and Water Supply and Sanitation Collaborative Council (WSSCC), kuandaa mkutano huo.

Mkutano huo kwa mtandao uliongozwa na Katibu Mkuu wa Giwa ambaye ni Rais wa Taasisi ya Divine Shakti, Sadhvi Saraswati, na kujadili mambo muhimu ya kiimani katika msimu huu wa Ramadhan wakishauri jamii kujilinda dhidi ya corona.

Makamu wa Mudiir na Mjumbe wa Bodi wa Jumuiya ya Ithna Asheri Tanzania, Shekhe Mohammed Abdi, alisema kukaa nyumbani ndiyo moja ya njia itakayosaidia kuokoa maisha ya watu kwa sababu hata Kurani inasisitiza watu kulinda maisha yao na ya wanaowazunguka. "Kusali nyumbani hakuwafanyi watu kutokuwa na imani lazima viongozi wa dini wahakikishe nyumba za ibada hazigeuki kuwa kitovu cha maambukizo ndiyo maana baadhi kwa sasa zimefungwa," alisema.

Imam wa Msikiti wa Ma'amur na Mjumbe wa Baraza la Ulamaa, Sheikh Issa Othman, alisema Baraza Kuu la Waislam Tanzania (Bakwata), limetoa miongozo inayotakiwa kufuatwa na misikiti yote ili kulinda waumini wanapokwenda kuswali nyakati hizi za virusi vya corona. Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Shekhe Khalid Ali Mfaume, alisema katika kipindi hiki ni muhimu viongozi wa dini kufanya kazi kwa pamoja na kuwajengea uelewa waumini dhidi ya corona.

"Wananchi wana wasiwasi na hofu, lakini viongozi wa dini tunao wajibu wa kuwalinda na kuwapa taarifa sahihi, ofisi yetu inatembelea misikiti ili kuhakikisha inazingatia miongozo kwa wanaosali wawe salama," alisema.

Katibu Mkuu wa Giwa, Bhagawati, alisema: "Mashirika ya kimataifa na ya dini wanapaswa kungana pamoja ili kuutokomeza na kuwaondolea hofu wananchi, kwa sasa haitakiwi kuwa na taarifa za kuwatisha wananchi bali kuwatia moyo," alisema.

Naye, Rais wa Parmarth Nikitan na mwanzilishi na mwenyekiti wa Global Interfaith Wash Alliance, alisema ni jambo la muhimu kufanya kazi na serikali na wadau wengine kama Unicef ili kuendelea kutoa ujumbe na kuwatia moyo wananchi kuhusu corona.

Mkurugenzi wa Kanda, Mpango wa Umoja wa Dini Afrika, Balozi Mussie Hailu, alisema wapo katika hatua ya mwisho ya kuwa na maombi ya pamoja Afrika ambayo yatawaleta kwa pamoja wadau wote.

# Umati yalia kisa kukosa madaktari

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (Umati) kisiwani Pemba, wameomba kupatiwa madaktari na vitendea kazi, ili kliniki yao ifanye kazi vizuri.

Ofisa Mipango wa Umati Pemba, Humoud Abdalla Humoud, alisema kliniki yao haifanyi kazi vizuri, kutokana na kukosa madaktari pamoja na vitendea kazi ambavyo ni vitu muhimu kwa chama chao.

Alisema ukosefu wa madaktari katika kliniki yao unasababisha wateja kukimbia na kutorudi tena kuendelea na huduma, kutokana na kuhisi kwamba usiri haukuzingatiwa.

Alieleza kuwa wanahitaji madaktari angalau wawili na vifaa vya uchunguzi, hatua ambayo itasaidia kutunza siri za wateja.

"Wateja wetu wengi ni vijana, na kama tunavyojua kwamba vijana mambo yao ni ya haraka haraka na usiri mkubwa, hivyo hawataki kupelekwa huko nakukaa muda mrefu bila kupata huduma," alisema.

# CWT yafunda walimu corona

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, kimewataka wanachama wake kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya corona ili iwe rahisi kuwakinga wanafunzi shule zitakapofunguliwa.

Aidha, CWT imesema kipindi hiki ni muhimu kwa walimu ambao wengi ni wazazi, kuwafundisha watoto wao kunawa maji tiririka kila wakati na sabuni wakiwa nyumbani, kuvaa barakoa ili wazoee.

Hayo yalisemwa na mwenyekiti mpya wa CWT wa Ruangwa, Raphael Soko, alipozungumza na gazeti hili na kuongeza kuwa kinga ni bora zaidi kuliko tiba.

Alisema, ugonjwa huo haujapata tiba wala chanjo, hivyo ni muhimu kuzingatia tahadhari na maelekezo ya serikali kama njia mojawapo ya kukabiliana nao.



Diwani wa Kata ya Rusoli, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, Boaz Nyehura (mwenye kofia), akishirikiana na wakazi wa Kijiji cha Buanga kumwagilia ukuta wa darasa la shule ya awali (shikizi), ya kijiji hicho juzi, inayojengwa kupunguzia watoto kutembea umbali mrefu kufuata elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sanamu ya Mwalimu Nyerere kujengwa makao makuu ya AU

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaratibu ujenzi wa sanamu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, katika viwanja vya jengo la Amani na Ulinzi la Julius Nyerere lililopo katika makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Akizungumza wakati wa uwasilishaji wa hotuba ya Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2020/2021 Bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema ujenzi wa sanamu hiyo ni utekelezaji wa Azimio la Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika jijini Harare, Zimbabwe mwaka 2015.

"Ujenzi wa sanamu ya Mwalimu Julius Nyerere katika Umoja wa Afrika (ni makubaliano ya mkutano wa wakuu wa nchi wa SADC ambao walikubaliana kuwa ujenzi huo lengo lake ni kutambua na kuenzi mchango wa waanzilishi wa SADC katika kulikomboa Bara la Afrika," alisema Dk. Mwakyembe.

Dk. Mwakyembe aliongeza kuwa ujenzi wa sanamu hiyo utatumia malighafi ya shaba nyeusi (bronze statue), na kuwa Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na Kamati ya Ujenzi wa Sanamu za Kuwaenzi Waasisi wa Taifa kama inavyotakiwa katika sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa ya mwaka 2004 zimeshaundwa na kuanza kazi tangu 2018.

Meneja Mradi wa mradi huo, Dk. Emmanuel Ishengoma, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Sanaa katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema hatua za awali za ujenzi wa sanamu hiyo zimeanza na mradi unatekelezwa na Kampuni ya SAMCRO ya Afrika Kusini chini ya usimamizi wa SADC na Tanzania, na utagharimu takriban Dola za Marekani 267,992.60 (Sh. 615,000,000) ambazo zitatolewa na SADC, na gharama za usimamizi kutolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Ishengoma aliongeza mradi huo unatarajiwa kukamilika Oktoba mwaka huu, ambapo sehemu kubwa ya kazi hiyo itafanyika Afrika Kusini, na ikiishakamilika na kuridhiwa na Tanzania pamoja na SADC itasafirishwa na kusimikwa katika Makao Makuu ya AU Addis Ababa, Ethiopia.

Ujenzi wa sanamu hiyo umetokana na wazo alilolitoa Rais wa zamani wa Zimbabwe, Hayati Robert Mugabe, katika Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC kuhusu mkakati wa kuwaenzi viongozi waanzilishi wa SADC ambao walishiriki katika kulikomboa Bara la Afrika.

# 'Vifaa kinga corona vihakikiwe ubora'

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amezita Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Viwango (TBS) na Mkemia Mkuu wa Serikali (GCA), kuhakikisha vifaa kinga na tiba vinavyoingizwa nchini vinahakikiwe ubora kabla ya matumizi.

Ummy alitoa kauli hiyo juzi alipopokea michango yenye thamani ya Sh. bilioni 2.1 ya vifaa tiba na kinga pamoja na fedha kutoka kwa wanachama wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF).

"Tunathamini michango yenu kwani upatikanaji wa vifaa kinga ni motisha kubwa kwa watoa huduma za afya ambao wapo mstari wa mbele katika mapambano haya nchini.

"Ninataka fedha zote zielekezwe kwenye akaunti ambayo ilishatangazwa hapo awali. Kuhusu vifaa, serikali ina wajibu wa kulinda afya za wananchi kwa kuhakikisha vifaa kinga pamoja na vifaa tiba vyote vinavyopokelewa, vinakidhi viwango vya ubora na usalama kulingana na mwongozo wa wizara wa msaada na vifaa tiba wa mwaka 2015.

"Hivyo, ninatoa wito kwa wadau wenye nia njema ya kuendelea kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya COVID-19, kuhakikisha kwamba, vifaa kinga na tiba vyote vitakavyoingizwa nchini, vihakikiwe ubora wake kabla ya matumizi na TMDA, TBS na CGA," aliagiza.

Waziri huyo pia aliwataka wenye viwanda nchini, kuzalisha kwa wingi vifaa kinga ikiwamo vitakasa mikono, barakoa pamoja na vifaa kinga vingine, ili serikali inunue kwa wawekezaji wa ndani kwa sababu mahitaji ni makubwa.

Ummy alisema serikali inatarajia kutoa mwongozo hivi karibuni wa matumizi ya barakoa za vitambaa vya kawaida katika ngazi ya jamii kwa ajili ya kujikinga.

"Hivi karibuni, tutatoa mwongozo wa matumizi ya barakoa za vitambaa vya kawaida katika ngazi ya jamii ili kuwawezesha wananchi kujikinga na maambukizo ya corona," alisema.

Waziri huyo alitoa wito kwa wazalishaji kuhakikisha wanashona barakoa hizo kwa kutumia mwongozo huo utakaotolewa ili kuwalinda wananchi.

Pia, aliwashukuru wadau wote wanaofanya jitihada za upatikanaji wa vifaa kinga kwa ajili ya watoa huduma za afya walioko mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya corona nchini huku akielekeza vifaa hivyo kununuliwa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

# Idadi wajawazito wanaohudhuria huduma za kliniki yaongezeka




Habari na Augusta Njoji

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imefanikiwa kuongeza idadi ya wajawazito 1,744,668 waliohudhuria kliniki wakati wa ujauzito.

Aidha, wajawazito 1,343,228 walitimiza mahudhurio manne au zaidi sawa na asilimia 77, ikilinganishwa na asilimia 41 kwa mwaka 2015/2016 wakati serikali ya awamu ya tano ikiingia madarakani.

Wizara hiyo ilitoa kauli hiyo jana bungeni katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Zainab Mussa Bakar.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya zahanati kutotoa huduma kwa wajawazito wanapoenda kuanza kliniki bila ya wenza wao.

"Je, serikali haioni kwamba tabia hii inaendeleza vifo kwa wajawazito kwa kukosa huduma hiyo?" Alihoji.



Katika majibu ya wizara hiyo, ilielezwa kuwa inaendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto, ikiwamo huduma kwa kinamama kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua.

Aidha, ilisema serikali imeendelea kutoa huduma kwa kinamama wakati wa ujauzito katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya, zikiwamo za kupimwa wingi wa damu, shinikizo la damu, magonjwa mbalimbali kama malaria, Ukimwi na kaswende.

"Lengo ni kutambua dalili za hatari au magonjwa wakati wa ujauzito, nakuchukua hatua stahiki mapema ili kuzuia matatizo yatokanayo na uzazi," ilisema wizara hiyo.

Vilevile, ilisema serikali inasisitiza wajawazito wote kuhudhuria kliniki mapema wakiwa na wenza wao ili kuweza kupata huduma hizo ndani ya muda muafaka.

"Kulingana na Sera ya Afya ya mwaka 2007, huduma za afya ya uzazi hutolewa bure bila malipo na huduma hizi hutolewa muda wote katika vituo vya kutolea huduma za afya," ilisema.

Kadhalika, ilisema huduma hizo hutolewa kwa kila mjamzito bila kujali kama amekwenda na mwenza wake au hakwenda.

Hata hivyo, ilisisitiza kwamba ni vyema mjamzito akaambatana na mwenza wake ili wapate elimu ya afya kwa pamoja na ikibidi wapate baadhi ya vipimo kwa pamoja ili kuhakikisha afya bora ya mtoto aliyeko tumboni.

"Ongezeko la wajawazito kuhudhuria kliniki ni kutokana na huduma nzuri zinazopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo watoa huduma za afya wanawahudumia wajawazito bila kujali kama wameenda na wenza wao ama hawakwenda nao," ilisema.

Wizara iliwataka wanaume kutambua juu ya umuhimu wa kuwasindikiza wenza wao pindi wanapohudhuria kliniki ya ujauzito.

# Mbunge ahoji miradi ya maji kutotoa maji



MBUNGE wa Tanga Mjini (CUF), Mussa Mbarouk, amehoji sababu ya baadhi ya miradi ya maji kwenye jimbo lake kutotoa maji, hali inayosababisha wananchi kukosa huduma hiyo.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema miongoni mwa mradi wa maji kwa vijiji 10 kwa kila halmashauri ni pamoja na mradi wa maji wa Mabokweni, Kiruku, Mpirani, Bwagamoyo hadi Chongoleani, ambayo haitoi maji.

"Mradi huu hautoi maji na wananchi wanaendelea kutaabika, je, tatizo ni nini?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema mradi wa maji Mabokweni uliopo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga ulisanifiwa kuhudumia vijiji/mitaa mitano (5) ya Mleni, Kibafuta, Mpirani, Ndaoya na Chongoleani.

Ilisema mradi huo unagharimu kiasi cha Sh. bilioni 2.41 utakapokamilika utawapatia huduma ya majisafi na salama wananchi wapatao 15,750.

"Mpaka sasa matangi mawili yamejengwa, ujenzi wa nyumba ya pampu na ufungaji wa pampu na umeme pamoja na ujenzi wa vituo 24 vya kuchotea maji umekamilika," ilisema.

Hata hivyo, ilisema hivi sasa, serikali kupitia Wizara ya Maji imeukabidhi mradi huo kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga kwa kuzingatia Sheria ya Maji namba 5 ya mwaka 2019 kwa ajili ya kuukamilisha na hatimaye kusimamia uendeshaji ili wananchi wanufaike na mradi huo.

"Hadi sasa, wananchi wapatao 2,500 wa vijiji vya Kibafuta na Kiruku wanapata huduma ya maji kufuatia kuunganisha maji katika vituo vitano vilivyopitiwa na mtandao," ilisema.

Aidha, ilisema mradi huo unatekelezwa kwa kutumia wataalamu wa ndani (Force Account) ili kukamilisha mradi huo kwa wakati na kwa gharama nafuu.



## MV. Mbeya II sasa yafanyiwa ukaguzi

BUNGE limeelezwa kuwa meli ya MV-Mbeya II ipo katika majaribio na ukaguzi kupitia Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC).

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Ludewa (CCM), Deogratias Ngalawa.

Katika swali lake, Ngalawa alihoji lini meli ya abiria itaanza kufanya kazi katika Ziwa Nyasa.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema ukaguzi huo utakapokamilika na kubainika kuwa unakidhi viwango vya kiufundi na usalama, itapewa cheti cha ubora na kuruhusiwa kuanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi huu.

Awali, ilifafanua kuwa serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imekamilisha ujenzi wa meli moja mpya iitwayo MV. Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 300 na mizigo tani 200 kwa wakati mmoja katika Ziwa Nyasa tangu mwezi Septemba, 2019.

"Kwa sasa meli hiyo ipo katika majaribio na ukaguzi kupitia TASAC, ni matumaini yangu kuwa, wananchi wanaoishi kandokando ya ziwa hilo watatumia fursa hii adhimu kusafiri na kusafirisha mazao na bidhaa zao ndani na nje ya nchi," ilisema.

Ilisema hali hiyo itaimarisha hali zao kiuchumi na kuinua uchumi wa nchi.




Ukurasa 12

Ijue ajira ya walimu nchini na CWT yao



Ukurasa 14

Watoto wavamia soko Morogoro, kuwaondoa jasho kwa manispaa

BUFE

IJUMAA MEI 8, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# NASAHA ZA RAIS JPM, WAZIRI MKUU KWA WATENDAJI WAKUU

• Walakini kukabili corona 'unatumbua' uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KINACHOTOKEA sasa kiko katika kumbukumbu za zama zinazohusika na mashairi ya ugonjwa corona, kutoka kila kona.

Kama ulivyo mfumo na maisha ya kibinadamu, jambo moja huzua mabadiliko katika lingine. Inapokuwa katika sura ya uchumi inabeba jina 'multiplier effect' ambayo ina tafsiri kubwa.

Maana inayobebwa jambo moja linazaa mengine. Mfano ni pale mwanafamilia akipata ajira, nyendo za mlo na kujiendeleza kwa wanafamilia unapanuka.

Inapofuatilia kwa kina mkasa wa corona nchini walau katika eneo dogo kuweka mantiki ndani ya walau maeneo mawili, moja kutoka kauli ya Rais Dk. John Magufuli akiwa nyumbani Chato na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, tayari kuna tafsiri kubwa, kiuchumi na kibiashara kitaifa.




Hapo ndipo kabla ya kupiga hatua zaidi kunapaswa kuzama katika maana zake za ujumla, kwamba uchumi unasimamia mantiki namna rasilimali kidogo zinavyoweza kukidhi mahitaji muhimu kwa kiwango cha juu kadri inavyowezekana.

Vivyo hivyo, biashara inabeba tafsiri ya shughuli za kubadilishana bidhaa au huduma kwa kiwango maalum cha mabadilishano ambayo ndio bei tajwa.

Ubora wa uchumi ni namna matumizi ya rasilimali yanavyokidhi kiwango cha juu cha matakwa sahihi ya jamii au mtu husika. Hapo biashara inapaswa kufanyika katika mfumo wa haki sawa kuwezesha malengo.

Huo ndio mzizi wa kuanzishwa Tume ya Ushindani Sawa katika Biashara nchini. Mchakato kuanzia taratibu za ununuzi hadi upande wa pili wa mauzo na taratibu zote za malipo, zinapaswa kuwa sahihi kitaaluma na kisheria. Kuna bodi inayohusika kusimamia ununuzi na nyingine ukaguzi wa hesabu ya umma (CAG).

Katika zama zilizopo za vita dhidi ya ugonjwa corona, Je, hizo zinafuatwa? Hapo inaanzia tafsIri ya uchumi kutumia vyema rasilimali za umma kukabili janga hilo linaloshambulia rasilimali muhimu katika uchumi, kwa maana ya watu.

Pia, kutetea makusanyo yatokanayo na kodi zao na kuwaweka huru kisaikolijia ili wazalishe.

Biashara nayo inafanyika katika mfumo na taratibu sahihi kitaaluma na kisheria, ili mwenendo wa kiuchumi uende katika mustakabali stahiki, mathlan kudhibiti mfumuko wa bei kutoka kwenye bidhaa za viwandani na vyakula?

Mapengo yanayojitokeza sasa nchini, alianza nayo kuainisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa hivi karibuni katika Ibada ya kitaifa jijini Dar es Salaam, alipoweka wazi hakuna uhaba wa sukari kitaifa na hata kiasi kidogo ambacho ni pengo kitaifa kilishaagizwa.

Hiyo ilitokana na kilichomshangaza ndani ya wiki kadhaa nchini bei ya sukari rejareja kuruka kutoka wastani wa Sh. 2,500 kwa kila hadi Sh. 4,000 na wananchi kuhangaika mno hadi sasa, huku katika ngazi ya juu si picha nzuri, kunakaribisha hali ngumu na mfumuko wa bei kwa wananchi.

Tayari kuna hatua zimeshachukuliwa kufuatilia hayo ya ubabaishaji katika biashara ya sukari, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kufuatilia sokoni 'mguu kwa mguu' na wanaopotosha bei kwa kurundika ghalani mzigo wachukuliwe hatua.

Ni tendo ambalo si mara ya kwanza kutokea na hata serikali ikachukua hatua inayostahili, dhidi ya wafanyabiashara.

Kurejea kwa Rais Dk. Magufuli, msomi wa kemia na hisabati za darasani, alionyesha kukerwa na baadhi ya hatua dhidi ya kukabili corona, zikiwa na athari za kiuchumi na kibiashara.

Anataja mbinu za kudhibiti ueneaji corona ikiwamo jijini Dar es Salaam, kwa kunyunyizia dawa mitaani, ambazo hakukubaliana nazo.

Katika ufafanuzi wake kitaalamu ulioendana na kauli ya kukemea, anasema haiendani kabisa na vita sahihi. Hapo inazaa maswali kutaka kuelewa mantiki ya ununuzi sahihi wa huduma hiyo imetokea wapi?

Katika taaluma na miongozo ya kisheria, ili ununuzi kufanyika, unapaswa kuwa na vitu vitano au inavyoeleweka katika taaluma hiyo '5 R' (Five Rights), kwa maana ya: Idadi kamili, ubora, chanzo, bei na muda sahihi.

Kwa kurejea kilichotamkwa na Rais Dk. Magufuli, kunazaa swali je, wahusika walifuata kanuni sahihi za ununuzi? Kwa maana kila ununuzi wa ofisi ya umma, una mtaaluma anayetumikia?

Pili, kwa mustakabali huo wa swali la Rais, inazua maswali hata katika matukio wa kanuni za fedha hadi kuidhinishwa malipo ya dawa hizo.

Kama ndani ya vita vilivyopo kukabili ugonjwa corona inafuatwa tafsiri ya uchumi 'namna bora ya kutumia rasilimali kidogo kwa manufaa makubwa kukidhi maslahi ya umma au watu" inaacha kitendawili kulikonI hatua hiyo kufikiwa?

Pia, kuna eneo ambalo Rais Dk. Magufuli amehoji umma kutishwa kwa kiwango cha juu kuhusu corona, ambayo haina tafsiri nzuri kwa ari na wajibu wao kujitokeza katika uzalishaji mali kitaifa.

Kwa mjumuisho, walakini katika kukabili corona, ina ishara mbaya kwa uchumi kitaifa.

UCHUMI

# Ijue ajira ya walimu na CWT yao

## • Katibu Mkuu aja na kabrasha lenye mafanikio




Walimu katika moja ya maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi ( Mei Mosi). **PICHA: MTANDAO**

**Na Renatha Msungu**

NI wiki moja imetimu, tangu kupita sherehe ya Mei Mosi, siku muhimu sana kwa wafanyakazi wote duniani, ikiwakumbusha mapambano ya kudai haki za maslahi bora katika sehemu zao za kufanya kazi.

Pia, ni siku muhimu kihistoria ya jamii ya wafanyakazi kukumbushana wajibu na haki katika ajira. Vyama vingi vya wafanyakazi vimekuwa vikitumia siku hiyo

kutoa matatizo kwa serikali na sekta binafsi, kutatua kero za wafanyakazi wake katika vitengo mbalimbali.

Chama cha WalimuTanzania (CWT), ambacho kiwawajumuisha katika ngazi mbalimbali, imeamua kutumia siku hiyo kujua majukumu yao, pamoja na kuyataja matatizo kitaifa katika imani kwamba kwa kiasi kikubwa inapata ufumbuzi wa umma.

Katibu Mkuu wa CWT, Mwalimu Deus Seif, anasema anaelekeza wito kwa walimu na wafanyakazi wengine kuendelea kuwajibika kwa manufaa ya taifa letu, akiwasisitiza kuendelea kujiunga kwenye vyama vya wafanyakazi, kwa vile imani ya siku zote 'umoja ni nguvu na mshikamano daima ndio ukombozi.'

"Tunapenda kusema, hakuna sababu ya wafanyakazi kubaki nyuma hususani walimu. Kinachotakiwa ni kujiunga na vyama mbalimbali ambavyo vinasaidia kujua haki zao za msingi katika masuala ya kazi," anasema Mwalimu Seif.

Anaeleza historia, kwamba CWT ilizaliwa mwaka 1993, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi nchini, ikilenga kutetea maslahi na haki za walimu nchini, hadhi ya taaluma ya ualimu na kuwapo vivutio vya kutosha, pia mazingira bora kikazi,

"CWT ni sauti ya walimu katika kufikisha ujumbe kwa watunga sera, wafanya uamuzi na jamii kwa ujumla juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya walimu na elimu kwa ujumla," anasema.

> **"Tunapenda kusema, hakuna sababu ya wafanyakazi kubaki nyuma hususani walimu. Kinachotakiwa ni kujiunga na vyama mbalimbali ambavyo vinasaidia kujua haki zao za msingi katika masuala ya kazi.**



Katibu Mkuu Chama Cha Walimu Tanzania, Mwalimu Deus Seif. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

**WANACHAMA**

Anafafanua Katiba ya Chama cha Walimu Tanzania, ni za aina nne, akiwataja kuwa wenye leseni za kufundishia;

wanachama shiriki, wanaogawanyika katika taaluma ya ualimu wanaishi na kufanya kazi nje ya nchi, wakufunzi katika vyuo vya ualimu na walimu wastaafu

Pia, anataka kuwapo wanachama wa heshima, ambao ni watu mashuhuri waliotoa mchango maalumu katika taaluma ya ualimu; mwisho ni wanachama maalum, ambao kimsingi ni waajiriwa wa CWT.

**HAKI ZAO?**

Mwalimu Grace Mahenge, kutoka Shule ya Sekondari Ngudu, mkoani Mwanza anafafanua haki za Mwalimu anazipata kutokana na kuwapo kwake kwenye chama, katika mtazamo ufuatao.

Huku akirejea katiba yake, anasema kushiriki katika ama kumchagua kiongozi au yeye kuchaguliwa katika nafasi ya uongozi ndani ya chama.

Hiyo inaendana na kuelimishwa maskahi yake ndani ya CWT na kupata fursa ya kutetewa katika shauri la kisheria linalohusu haki zake, anajitetea, hata kukata rufani anapokuwa na dhamira hiyo.

Pia, Mwalimu Grace anasema kuna nafasi za kushiriki na kufaidi matunda yatokanayo na kazi za chama kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa.

Hata hivyo, kama ilivyozoeleka katika hatua nyingine, mengi yana upande wa pili wa shilingi, kwamba mwanachama anaweza kuadhibiwa na hata kufutwa uanachama, pindi anapoenda kinyume na taratibu.

Katibu Mkuu, Seif anaendelea kufafanua kuwa, chama hiki kimefanikisha malengo ya kuanzishwa kwake mpaka sasa?

**CWT IMEFANIKIWA?**

Ni swali amabalo Nipashe ilimuelekezea Katibu Mkuu Seif, anayejinasibu kufanikiwa kuwaunganisha walimu wa ngazi mbalimbali, akitaja mifano ya elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vya maendeleo ya wananchi na wadhibiti ubora.

Eneo jingine analolitaja, ni utoaji mafunzo kwa viongozi na wanachama kuhusu stadi za uongozi, ufundishaji bora wa masomo ya Kiingereza, Hisabati, Sayansi na Walimu ya Mazingira kwa shule za msingi.

Huku akiendelea kuhusu mengine : "Kujenga uwezo wa ufundishaji somo la uraia kwa shule za sekondari, mafunzo ya diploma ya elimu ya awali kwa walimu wa shule za msingi. Semina kwa maofisa elimu na maofisa elimu taaluma wa mikoa na wilaya wa nchi nzima."

Kwingine Seif anakojivunia ni mafanikio ya utetezi wa wanachama wake, manufaa ya ushauri na utetezi wa kisheria katika matatizo yanayohusiana na mishahara na madaraja kazini, malipo ya likizo, uhamisho, pensheni na mirathi na matibabu.

"Pia kimeshughulikia utatauzi wa kero ya Walimu wa Shirika la Elimu Kibaha, walioathiriwa na Waraka Namba Mbili wa mwaka 2010 wa Msajili wa Hazina, ambao utekelezaji wake uliwafanya walimu wapya kuwazidi mishahara walimu wa zamani kwa ngazi mbili.

"Suala hili limepatiwa ufumbuzi, ingawa bado kuna changamoto zinazoambatana na marekebisho hayo ambazo zinaendelea kushughulikiwa," anasema.

Seif anasema mwaka 2003, kilipatikana chombo cha majadiliano kisheria (Public Service Negotiating Machinery Act, 2003) kwa maslahi stahiki ya walimu

Pia, anaorodhesha kitega uchumi cha jengo la ghorofa, maarufu Mwalimu House, jijini Dar es Salaam na kununuliwa vyombo vya usafiri kwa ofisi zote za mikoa na wilaya, kuwezesha kufikia walimu kirahisi na kutatua changamoto zao

Kuna malipo? Katibu Mkuu anafafanua: "Posho za madaraka kwa maofisa elimu kata, wakuu wa shule na walimu wakuu."

**SAUTI YA MWALIMU**

Mwalimu John Kiliani, anasema CWT imekuwa ikifanya mikutano na mazungumzo ya kila mara na serikali ambayo ndio mdau mkuu wa elimu na mwajiri mkubwa wa walimu.

"Mikutano na mazungumzo hayo yamekuwa yakilenga katika kuboresha mishahara, madaraja, ulipwaji malimbikizo ya mishahara," anasema na kutaja, mengine yanayoendana nayo kuwa ni:

"Upatikanaji nyumba za walimu, ulipwaji madeni yasiyo na mishahara na uboreshwaji mazingira ya kufundisha na Kujifunzia."

**BENKI NAFUU**

Pia, CWT katika orodha yake ya mafanikio, anataja mafanikio ya kuanzisha benki, yao inayoleta unafuu wa kiuchumi na kuwepo akaunti na huduma mbalimbali zenye tafsiri bora kwa maslahi ya walimu.

"Kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, ndugu Anthony Mtaka, CWT imechangia fedha katika mfuko ulioanzishwa na Mkuu wa Mkoa, kuwakopesha walimu kwa riba nafuu na kuwaondoa katika makucha

ya wakopeshaji binafsi waliokuwa wanawadidimiza walimu kwa riba kubwa zisizolipika na wakati mwingine kushikilia ATM zao,"anasema Katibu Mkuu .

UCHUMI

# Mstaafu EAC asimulia safari ya robo karne kufuatilia mafao yake

**Na Anthony Gervas,** MWANZA



Mkazi wa wilaya Sengerema, Mwanza, Mzee Festus Mkuli. **PICHA: NA ANTHONY GERVAS**

"NILISTAAFISHWA kwa manufaa ya umma mwaka 1994, nilipokuwa mfanyakazi wa Idara ya Ushuru na Forodha mkoani Mwanza, ambayo sasa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Hadi sasa sijalipwa mafao yangu na serikali, kuanzia kufanya kazi Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)," anadai Mzee Festus Mkuli (80), mkazi wa wilaya Sengerema, mkoani hapa, alipokuwa na mazungumzo maalum na Nipashe jijini hapa.

Anaendeleza simulizi kwamba baada ya kustaafishwa kazi, alianza kuugua na mwaka 1998 huku akiendelea kudai mafao serikalini, akitaja kuwa ya aina mbili, ikiwemo kutoka EAC.

"Niliendelea kufuatilia mafao yangu yote kwa njia ya barua, kwa sababu nilikuwa mgonjwa kuanzia utumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu mwaka 1975 hadi 1977 ilipovunjika," anasema na kuendeleza simulizi kwamba:

"Ni pamoja na yale ya kustafishwa kazi kwa manufaa ya umma mwaka 1994, wakati nikifanya kazi katika Idara ya Ushuru wa Forodha mkoani Mwanza,"

Mzee Mkuli anasema, baada ya EAC kuvunjika serikali nchini ilitangaza ajira zao ni endelevu na walipangiwa kazi katika mashirika yaliyoundwa, ikiwamo Idara ya Ushuru na Forodha.

Anaeleza ufuatiliaji wa mafao yake tangu mwaka 1998 hadi sasa hauna mafanikio kutika kwa mhusika Idara ya Hazina, iliyo wajibika na malipo ya wastaafu wa Idara ya Ushuru na Forodha wa EAC.

Mstaafu huyo analalamika kwamba, madai yake yamepitia ngazi mbalimbali serikalini, ikiwamo kwa wajiri wakati huo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Ofisi ya Hazina.

Pia, anataja kwingineko ni kwa Katibu Ikulu Mkuu Kiongozi Ofisi ya Rais, Ikulu mwaka jana iliyoielekeza ofisi ya Katibu Mkuu Hazina, kutekeleza, lakini analaamika hajafanikio.

Aidha, analalamika kupitia ngazi mbalimbali, ikiwamo kuandika barua kwa Kamishna wa Idara ya Ushuru na Forodha, kuhusu ushahidi wa kustaafishwa kwake kwa manufaa ya umma mwaka 1994.

Mzee Mkuli, anadai alipokuwa mkoani Mwanza, aliandika barua TRA na nyingine ni katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini. Hakufafanua hatua zilizofikiwa.

### SIMULIZI KUSTAAFU

Mzee Mkuli anaeleza kwamba baada ya kustaafishwa kazi serikalini, alirejea kijijini kwake Sengerema akijishughulisha na kilimo, huku akiendelea kufuatilia mafao yake, hadi alipoanza kuugua ndiko alipokwama.

Kwa sasa, Mzee Mkuli analalamika ameishia katika ufukara, akilalama barua zake tatu tofauti kudai mafao kwa mwajiri wake, Kamishna wa Idara ya Forodha hazikuambulia mafanikio.

"Mimi naiomba serikali kupitia Hazina, iangalie madai ya mafao yangu inisaidie kunilipa," anaomba Mzee Mkuli.

### BARUA HAZINA

Barua iliyoandikwa kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Hazina ya Novemba 14 mwaka juzi, ina maelezo kwamba:"Umedai kuwa uliajiriwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Idara ya Ushuru na Forodha (Customs and Excise), ambayo leo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Aprili mwaka 1975.

"Umeendelea kudai kwamba ulistaafishwa kwa manufaa ya umma Juni 30 mwaka 1994 na hadi leo hujalipwa mafao ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika Juni 1977....

"Umedai kwamba vyombo vya habari (magazeti) mwaka 2008 vilieleza kwamba mafao ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki yalilipwa na kwamba serikali ilikuwa inalipa na mapunjo. Umeendelea kueleza kwamba 2011 ulihabarishwa tena kwamba mapunjo yalikuwa Sh. Bilioni 117 ..." inaeleza sehemu ya barua kutoka serikalini.

Kwa mujibu wa barua hiyo, wafanyakazi hao walienda mahakamani na kufungua kesi dhidi ya serikali, wakidai mafao yanayotokana na utumishi wao EAC.

Inaelezwa kesi pande hizo mbili ziliafikiana na kuunda kamati ya majadiliano na wafanyakazi na wakaafikiana, kisha zikaunda hati ya makubaliano iliyosajiliwa mahakamani, kuhitimisha kesi ya mwaka 2003 iliyofunguliwa na wafanyakazi.

Barua ya Hazina inayoanzia waraka kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, ilielekeza kulipwa mafao hayo kwa kuzingatia hati ya makubaliano na sheria za EAC.

"Sheria za fedha na kanuni zake, waliohusika kulipwa mafao hayo ni waliokuwa wafanyakazi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wapatao 31,831 na kiasi kilichokubaliwa pande zote mbili ni Sh. bilioni 117 tu" anasema Katibu Mkuu, katika batua yake.

Baada ya hapo, inaelezwa Wizara ya Fedha na Mipango, ilianza kulipa mafao kwa wastafu wa iliyokuwa EAC Septemba mwaka 2005 kama ilivyo hati ya makubaliano.

> **Mwaka 2018 juni 30, nilipeleka pia malalamiko yangu Ofisi ya Rais, mwaka 2018 Julai 25, nilipeleka kwa katibu Mkuu Ikulu, alijibu kwa kumuagiza Katibu Mkuu Hazina atekeleze.**

Aidha, inaelezwa wastaafu waliokamilisha taratibu zilizohitajika walilipwa mafao kwa kuzingatia sheria na kanuni za pensheni zilizotumika katika iliyokuwa EAC.

Inaelezwa, taarifa ya utekelezaji uamuzi uliwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri mnamo Julai 15 mwaka 2010 liliyoomba kupokea taarifa ya utekelezaji na kutoa kibali cha hitimisho la ulipaji mafao, kwa sababu lisingeweza kuendelea bila ya ukomo.

Pia ilielezwa, pamoja na kuhitimishwa malipo hayo, Wizara ya Fedha ilielekezwa kuendelea kushughulikia madai yatakayojitokeza, kwa kutumia sheria na taratibu zilizotumika.

Hivyo, Wizara ya Fedha ilitekeleza maelekezo kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji.

"Katika barua yako wewe hujaeleza kama wewe uliwasilisha madai yako kwa aliyekuwa mwajiri wako katika kipindi cha kuanzia 2005 hadi 2010, kwani malipo hayakuwa yanafanyika bila kufuata sheria na kanuni za fedha," alisema Katibu Mkuu Hazina.

### MDAI MAFAO

Mzee Mkuli anasema, alidai mafao yake kwa mwajiri kwa mara ya tatu mwaka 2006 bila ya mafanikio na mwaka 2010 aliandika barua kwenda Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora, Novemba mwaka 2016.

Pia, anasema alipeleka malalamiko yake TRA mkoa Mwanza na mwaka uliofuata alifikisha katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, akiendelea:

"Mwaka 2018 juni 30, nilipeleka pia malalamiko yangu Ofisi ya Rais, mwaka 2018 Julai 25, nilipeleka kwa katibu Mkuu Ikulu, alijibu kwa kumuagiza Katibu Mkuu Hazina atekeleze."

Mstaafu huyo anadai Katibu Mkuu Hazina alijibu bila ya kutekeleza na ndipo alipolalamika tena Mei, mwaka jana, kwa Ofisi ya Katibu Mkuu Kiongozi, iliielekeza Ofisi ya Katibu Mkuu Hazina kwa mara ya pili, kutekeleza maelekezo ya Ikulu.

"Mwaka 2019 Julai, Katibu Mkuu Kiongozi aliniagiza mimi mwenyewe nipeleke kumbukumbu za ajira zangu kwa Katibu Mkuu Hazina, ambazo mwaka huu 2020 Januari 26 nimefanya hivyo," anaeleza Mzee Mkuli.

Kwa sasa Mzee Mkuli, anaeleza hofu yake ni kutopata mafao yake anayoangalia kwa wastani unakaribia kwa miongo kadhaa.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa anwani ya baruapepe: anthonygervas@yahoo.com na simu (+255) 0682 869,244 Kanda ya Ziwa.***

BIASHARA

KIBARUA CHA 'LIKIZO YA COVID 19'

# Watoto wavamia soko Morogoro, kuwaondoa jasho kwa manispaa

- Tangu 2017 hadi zama corona wamo
- Mkurugenzi: Safari hii wazazi mmo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KATIKA kata ya K'ndege, mjini Morogoro, kuna shida inayolalamikiwa ya kuibuka wimbi la ajira ya watoto ndani ya manispaa yao.

Mwenyekiti Msaidizi wa Soko la Mawenzi lililopo katika kata hiyo, Peter Lyoba, anasema ajira hiyo ya watoto kwa sasa inakinzana kwa kiasi kikubwa na maradhi ya corona, hasa ikirejewa malekezo ya kiserikali, juu ya namna ya kuishi.

Baadhi ya hatua ambazo zimeshachuliwa kuhakikiksha umma usichanganyike, shule na vyuo vyote vimeshafungwa kwa zaidi ya mwezi mmoja, huku Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiusihi umma kutokuwa na safari zisizo na ulazima.

Lyoba anasema, uamuzi wa marufuku kwa watoto sokoni K'ndege ni wa muda mrefu uko tangu mwaka 2017 na janga la corona, limechangia kukazia uamusi huo.

Anasema waliweka utaratibu wa kuwapokea vijana waliofikia umri wa kuanzia miaka 18 sokoni kwa ajili ya kufanya biashara ndogo, kutokana na kuwapo wimbi la wenzao wenye umri mdogo kuvamia soko kufanya uchuuzi.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Msaidizi huyo, vijana hao wadogo walijihusisha na ujasiriamali wa mifuko, maji na wengine kubeba mizigo ya wateja, kwa ujira mdogo.

Anasema, baada ya kupata ushirikiano kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya K'ndege, Aziza Omari, aliyewezesha kuwatambua vijana hao na wamefanikiwa kuwapa jezi 35 wenye umri kuanzia miaka 18, watambulike rasmi na wengine wanaozurura wanachukuliwa hatua.

Ofisa Mtendaji Aziza, anafafanua kwamba, idadi ya kundi hilo linalovamia soko wenye umri chini ya miaka 18, idadi yao ni wastani wa 25, shughuli yao kuu ni kuuza maji na kusaidia shughuli ndogo za wafanyabiashara kama vile kupanga ndizi mezani, baada ya kuzishusha kutoka kwenye gari.

Aziza anasema, mkakati wa hivi sasa ni mahsusi kuwanusuru na maradhi ya corona, yanayaotikisa nchi hivi sasa.

Anasema kuanzia mwaka jana waliendesha operesheni ya kuwakamata watoto hao, wakishirikiana na mgambo wa manispaa na waliwanasa watoto 21 kutoka kata za Misufini na Chamwino ndani ya manispaa, pia kutoka Mgeta, wilayani jirani ya Mvomero.

Anasema, baada ya kuwakamata watoto hao, waliwaita wazazi wao na kuwaeleleza wawaridushe makwao na wawe katika matunzo yenye uangalizi makini na anayetoka Mgeta, walibeba jukumu la kurejesha.

Hivi sasa katika mlipuko wa ugonjwa corona, wameweka mikakati kwa kushirikiana na uongozi wa soko na magambo, kuwakamata watoto wote wanaozagaa sokoni.



Makamu Mwenyekiti wa Soko la Mawenzi, Peter Lyoba, akimuelimisha mtoto, Hussein Mkude, aliyekuwa akiuza maji sokoni hapo, juu ya madhara ya kutembea kwenye mikusanyiko na maradhi ya corona yanayoitikisa dunia. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

> **"Pia, inaenda mbali kwa kutaka ajira ya mwenye umri chini ya miaka 18, iwe katika kazi nyepesi pekee, ambazo haziwezi kuwa na madhara kwa afya ya mtoto na maendeleo yake.**

**NINI CHANZO?**

Mmoja wa watoto wenye umri chini ya miaka 18 (jina tunalo) anayeishi katika Manispaa ya Morogoro na mwanafunzi wa darasa la saba, anasema amekuwa akiuza maji sokoni katika kipindi cha likizo na siku za mwisho wa wiki.

Mtoto huyo anakiri kujua vyanzo vya maambukizo vya corona, ni mtu kuwa kwenye mazingira ya msongamano na kugusana, analazimika kufanya biashara yenye mazingira hayo, kutokana na agizo la mama yake.

Mwenyekiti wa Soko la Mawenzi, Ramadhani Mohamed anapokea hoja kwa kutokukubaliana na mtazamo wa mtoto huyo, akisema soko lina wafanyabiashara zaidi ya 1000 na wateja wa kila siku zaidi ya 3000, hivyo watoto kuendelea kuwapo ni kuwakaribishia hatari kiafya.

Anatumia fursa hiyo kuwaagiza wazazi, kutilia mkazo maagizo ya kiserikali, likiwemo la kuwataka watoto watulie majumbani.

Justina Anthony, mfanyabiashara sokoni anayeishi Kihonda mjini hapa, anakiri kuwapo wachuuzi wenye umri chini ya miaka 18 sokoni na anapowahoji, wanajibu "biashara hizo zinasaidia familia zao ambazo hazina fedha kutokana na kufiwa na mzazi mmoja."



Mwenyekiti wa Soko la Mawenzi, Ramadhani Mohamed, akiendelea na ugawaji wa ndoo za kunawa maji kwa wateja na wauzaji, ili kujikinga na corona kwenye soko hilo.

Anaeleza marejesho yake ya utashi wa uzazi alio nao, huwataka watoto hao katika nyendo hizo za kutafuta riziki, wazingatie kanuni za usafi katika zama iliyopo ya corona, ikiwamo kunawa mikono kila mara kwa sabuni na maji tiririka.

Hata hivyo, anawataka wazazi wenzake kutambua kuwa watoto wanapaswa kutulia nyumbani na sio kuwatuma sokoni pale wao wanapohitaji bidhaa.

**MANISPAA MORO**

Ofisa Habari wa Manispaa Morogoro, Lilian Heneriko, akizungumza kwa niaba ya, Mkurugenzi wa Manispaa, anasema watoto hao wamekuwa wakirudi sokoni kila mara, licha ya hatua ya kuondolewa kila mara

Lilian anasema, mkakati wa sasa wa manispaa ni kuendesha operesheni 'kamata kamata' kwa kuwatumia mgambo wa manispaa na kisha wanafikishwa polisi, ambako kila mzazi atawajibika kwenye vyombo vya dola.

Ofisa Mratibu wa Vilabu vya Jinsia Shuleni kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP- Mtandao), Joyce Mkina, anasema kuna changamoto watoto wanaingia kwenye maeneo ya mikusanyiko kama sokoni, huku wazazi wanakosa umakini kuwakinga na maradhi kama corona.

"Kuna uhaba wa elimu ya kuwalinda watoto wadogo kwa sababu bado hawajui kama vile corona inawapata watu wazima tu na sio watoto.


"Ukweli ni kwamba wenyewe ni wahanga namba moja kama walivyo watu wazima," anasema Joyce, anayerejea maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Anasema wana mkakati wa kuelimisha watoto, ambao awali ilitumika kuwaelimisha ukatili wa kingono kwa mafanikio na sasa wanalenga kurekodi video fupi za watoto wakielimisha wenzao, ili zitawanywe katika maeneo mbalimbali ya nchi. Pia, ofisa huyo anasema hivi sasa asasi ya TGNP- Mtandao inawahimiza wazazi kuendelea kuwalinda na kuwaelimisha watoto kutokana na janga la ugonjwa huo.

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004 ina miongozo ya sera za ajira, inazuia ajira ya mtoto chini ya miaka 14.

Pia, inaenda mbali kwa kutaka ajira ya mwenye umri chini ya miaka 18, iwe katika kazi nyepesi pekee, ambazo haziwezi kuwa na madhara kwa afya ya mtoto na maendeleo yake.

Sera ya Ajira nchini, inazuia kuajiriwa mtoto kamwe kusimzuie kuhudhuria masomo shuleni, kushiriki kwenye ufundi stadi au miradi ya mafunzo yaliothibitishwa na mamlaka yenye madaraka au uwezo wa mtoto kufaidi maelekezo anayoyapata.





# Wafanyabiashara wakubwa waonyeshwa fursa ya madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wakubwa nchini wametakiwa kuchangamkia fursa ya ununuaji wa madini yaliyopo kwa wachimbaji, baada ya serikali kulegeza masharti kutokana na janga la ugonjwa wa corona.

Rai hiyo ilitolewa na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (Femata), John Bina, alipokuwa akizungumza na Nipashe kutokana na athari za virusi vya corona kwenye sekta ya madini.

Alisema serikali imeruhusu mtu yeyote mwenye mtaji wa kununua madini afuate taratibu zilizowekwa, na imeondoa baadhi ya vizuizi kwa wanunuzi kununua kwenye masoko ya madini.

Rais huyo alisema ugonjwa huo umeathiri soko kwa kuwa madini mengi huuzwa nje ya nchi.

"Tumefanya jitihada sisi shirikisho kwa kushirikiana na wizara, tumeshawishi benki na watu binafsi na tumeondoa masharti ili kununua madini... soko la dhahabu duniani limepanda sana, lakini soko letu limebaki pale pale kwa kuwa wanunuzi wengi wapo nje na hakuna ndege ya kwenda kule," alisema.

Aliwashawishi wanunuzi wenye uwezo mkubwa kifedha kuendelea kununua madini kwa kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.

"Tunashukuru baadhi ya maeneo kama Chunya fedha zimeanza kwenda kununua dhahabu, tunaendelea kushawishi wafanyabiashara wenye fedha ili kutoa unafuu, na tupo makini tunazungumza kwa njia ya mtandao ili kuondokana na athari hiyo," alisema Bina.

Aliwataka wachimbaji kufuata masharti na maelekezo yanayotolewa na serikali namna ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.

Katika hatua nyingine, Bina aliwataka wanasiasa kuacha kumwingilia Rais John Magufuli kwenye majukumu yake kipindi hiki cha kukabiliana na ugonjwa huo.

Bina alisema urais sio jambo dogo na haipaswi kila wakati kuonyesha kutetemeka na kuwatisha wananchi wakati hatua mbalimbali zinachukuliwa na serikali kudhibiti ugonjwa huo.

"Unaweza ukadhani ni kitu kidogo ukapewa ukaanguka, Rais ni kiongozi anapokuwa ni kiongozi sio aonyeshe kutetemeka. Hata katika familia mimi naweza kuliona tatizo, lakini siwezi kusema tutakufa na njaa, huyo ndiye kiongozi, wale wanaotaka Rais atoe takwimu za vifo, kulitisha Taifa lake si sahihi," alisema.

# Waziri azitaka mamlaka za maji kutoa elimu usomaji wa ankara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ameziagiza mamlaka za maji nchini kutoa elimu ya usomaji wa ankara za maji kwa wateja wake ili kuondokana na manung'uniko ya kulipishwa gharama kubwa za matumizi ya maji.

Aweso alitoa kauli hiyo kufuatia malalamiko mengi ya wananchi kuhusu malipo ya ankara za maji kutolingana na matumizi halisi ya maji, katika ziara ya kukagua mradi wa maji Chamwino.

Alisema elimu hiyo ikitolewa itapunguza malalamiko hayo.

"Nimebaini tutapunguza malalamiko mengi ya wateja, endapo tutaanza utaratibu wa kutoa elimu tunapokuwa tunafika kusoma mita kwenye nyumba za wateja wetu... wengi wao hawana ufahamu na kusababisha mwamko mdogo wa kulipa ankara zao kwa wakati," alifafanua Naibu Waziri Aweso.

Alizitaka mamlaka hizo kuhakikisha zinatoa elimu hiyo juu ya mita wanazofungia wateja jinsi zinavyofanya kazi, matumizi ya mteja husika na gharama za kila uniti ili kujenga uaminifu kwa wateja.

Akizungumzia kuhusu mradi wa maji Chamwino, Aweso alisema wizara itatoa Sh. milioni 700 wiki ijayo kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi wa tangi la maji la ujazo lita milioni 2.5 na ununuzi wa pampu za mradi huo.

"Mradi huu utagharimu Sh. milioni 855 kwa awamu ya kwanza na shilingi bilioni 1.16 kwa awamu ya pili, una lengo la kuimarisha huduma ya majisafi na majitaka kwa asilimia 95 katika Jiji la Dodoma, Mji wa Chamwino na maeneo ya pembezoni mwa jiji kwa miaka 30 ijayo," alisema Aweso.



Mchuuzi wa mapera akitafuta wateja katika eneo la Madukani, jijini Dodoma jana. Wachuuzi wengi wa matunda hayo hutembea kwa miguu umbali mrefu kutoka vijiji vya Mvumi, Handali wilayani Chamwino na kwenda katika Jiji hilo kusaka wateja. Pera moja linauzwa kwa Sh. 200 hadi 500. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake wapewa somo kuhusu dawa ya udumavu kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAWAKE wa Mkoa wa Dodoma, wameshauriwa kuhakikisha wanawapatia lishe bora watoto wenye umri wa miaka sifuri hadi mitano ili kuondokana na tatizo la udumavu.

Kwa mujibu wa Ofisa Lishe mkoani hapa, Hariet Caren, kwa mwaka 2010 udumavu ulikuwa zaidi ya asilimia 50 na mwaka 2015 ulishuka na kufikia asilimia 36.5, lakini kwa mwaka 2018 ni asilimia 37.2 ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.7.

Akizungumzia chanzo cha udumavu, Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Halima Kassim, alisema unatokana na mtoto kukosa lishe bora kwa kipindi kirefu.

"Dalili za udumavu ni kuwa na kimo kifupi kulingana na umri wake, na sababu za watoto kuwa na udumavu ni lishe duni, mtoto kuugua mara kwa mara katika kipindi cha siku 1000 za maisha yake, taratibu duni za ulishaji watoto wachanga, na inatokana na kutopewa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita," alisema.

Alishauri wanawake kabla ya kupata ujauzito wahakikishe wanakuwa na afya njema na baada ya kuwa wajawazito wahakikishe wanapata lishe bora hata baada ya kujifungua.

Januari, 2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilisaini mikataba na wakuu wa mikoa kusimamia lishe kwenye maeneo yao, kwa lengo la kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto.

# TBL yamkabidhi RC Mbeya vifaa vya millioni 20/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL), imetoa msaada wa vitakasa mikono lita 500 kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ili visaidie kukabiliana na janga la Covid-19 ambalo linaitesa dunia kwa sasa.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, meneja uzalishaji wa kampuni hiyo, Godwin Fabian, alisema vina thamani ya Sh. milioni 20 na vimetolewa kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Fabian alisema vifaa hivyo vitakuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa mkoa huo hususani wasio na uwezo wa kumudu gharama za kununua vitakasa mikono.

"Tumeamua kuunga mkono jitihada za serikali katika vita hivi dhidi ya corona kwa kutoa msaada wa vitakasa mikono lita 500, tunaimani itasaidia kukabiliana na ugonjwa huu," alisema Fabian.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyata, alisema vifaa hivyo vitasaidia kupunguza maambukizo ya virusi vya corona na kuwaomba wadau wengine kuchangia sekta ya afya ambayo ina uhitaji mkubwa. Dk. Manyata alisema bado kuna mahitaji ya vifaa tiba na vya kunawia kwa watoa huduma wa maeneo mbalimbali ya mkoa kwa kuwa vilivyopo havikidhi mahitaji. Akipokea msaada huyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema vifaa hivyo vitagawiwa kwenye maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii ikiwamo hospitali, sokoni na sehemu zenye uhitaji.

Alitoa rai kwa watu wengine ambao wanatamani kuunga mkono jitihada za serikali dhidi ya ugonjwa wa corona kusaidia vifaa mbalimbali vya kunawia pamoja na vifaa tiba.



Baadhi ya wajasiriamali wa eneo la Kiwila, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wakiwa wamejitwisha ndizi, wakisubiri wateja ambao ni abiria wa kwenye magari, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Wakulimawalia soko la ndizi kudorora

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WAKULIMA wa ndizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wamelalamikia kukosa soko la uhakika, kutokana na wateja ambao wengi wao wanatoka nje ya nchi ikiwamo Afrika Kusini, Malawi na Congo kutoingia nchini kutokana hofu ya maambukizo ya virusi vya corona.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Ezekiel Mwakota, wakati akizungumza na Nipashe kuwa kwa sasa hali ya soko la ndizi sio ya kuridhisha kutokana na zao hilo kukosa kabisa wateja.

Alisema sababu kubwa iliyochangia zao hilo kukosa wateja ni ugonjwa wa Covid-19 ambao umesambaa nchi mbalimbali hali iliyosababisha mipaka na shughuli nyingine kufanywa kwa tahadhari kubwa pamoja na utoaji wa maalum wa vibali.

"Soko la ndizi limeanza kuporomoka kwa sababu wanunuzi wengi wa zao hilo kutoka ndani na nje ya nchi hakuna kutokana na hili janga la corona wakulima wengi wanapata hasara kwa kuwa muda mwingine wanalazimika kupungua kutokana na hofu ya uwapo wa virusi vya ugonjwa wa corona," alisema Mwakota.

Alisema zao la ndizi wilayani humo linachangia kwa kiasi kikubwa pato la halmashauri, hivyo kudorora kwake kutasababisha mapato kushuka na kukwamisha shughuli nyingine za maendeleo ambazo zinategemea ushuru wa zao hilo.

Alisema asilimia 90 ya wakazi wa wilaya hiyo inategemea kilimo cha ndizi kuendesha maisha yao hivyo kudorora kwa soko kunaumiza makundi mbalimbali.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Benedict Abraham, alisema hali ya sasa kiuchumi ni mbaya zaidi kwa sababu hakuna wateja hata wanaofika kwenye magulio yao.

Alisema kipindi cha nyuma walikuwa wanachumbia (wekeza) ndizi mashambani kutokana na wingi wa wateja, lakini kwa sasa ni tofauti badala yake wateja wanaowategemea ni mama lishe pekee.

Naye Donald Mwasanga alisema maisha yake kwa sasa yanategemea kilimo cha ndizi hivyo kukosekana kwa soko ni pigo kwa sababu hana shughuli nyingine ya kumwingizia kipato.

# Maji Makambako yaibuka kinara utoaji huduma

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Makambako mkoani Njombe, imeibuka kinara katika utoaji wa huduma kati ya Mamlaka za maji za wilaya na miji midogo 83 kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2018/19.

Hayo yalibainishwa jana jijini Mbeya na Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), Karim Ally, wakati wa utoaji tuzo kwa mamlaka zilizofanya vizuri.

Alisema kwa upande wa mamlaka za miji ya wilaya na miji midogo zilizofanya vizuri, iliyoshika nafasi ya kwanza ni Mamlaka ya maji katika Mji wa Makambako, ushindi ulitokana na juhudi zao katika kuwahudumia na kuwapatia wakazi wa eneo hilo maji ya uhakika.

Alifafanua kuwa nafasi ya pili katika tuzo hizo ilichukuliwa na Mamlaka ya Maji Mikumi, huku Mamlaka ya Maji Biharamulo ikishika nafasi ya tatu.

"Leo hii nawakabidhi rasmi Mamlaka ya Majisafi na Usafi na Mazingira Makambako tuzo mbili na vyeti vitatu kutoka na kazi nzuri wanayoifanya katika utoaji huduma bora za majisafi na usafi wa mazingira," alisema.

Ally alisema tuzo hizo na vyeti kwa mamlaka bora katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa mwaka wa fedha wa 2018/19 ni miongoni mwa mamlaka 83 za maji za wilaya na miji midogo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Makambako, Mhandisi Lufyagile Oscar, alisema tuzo na vyeti vilivyotolewa na Ewura vimechochea ari ya kufanya kazi kwa bidii na watahakikisha mwaka 2020/ 2021 watashinda tena.

Alisema moja ya sababu mamlaka hiyo kushinda ni kuwasikiliza wanachokihitaji wateja na kuwatatulia vikwazo vinavyowakabili.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji wa Makambako, Paulo Malala, aliishukuru Ewura kwa kutambua mchango wao mkubwa katika kutoa bora ya majisafi na salama kwa wananchi.

Malala alisema tuzo na vyeti vilivyotolewa vitasaidia Mamlaka ya Mji Makambako kujijenga zaidi kwa mwaka unaokuja na kujipanga katika utoaji wa huduma kwa wananchi.





# SMZ yatakiwa kuzingatia sheria ajira kwa watu wenye ulemavu

**NaRahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imetakiwa kuzingatia masharti ya sheria zake na matakwa ya mikataba ya kimataifa kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaajiriwa serikalini na katika sekta binafsi kwa mujibu wa sifa na vigezo.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, wakati akichangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema licha ya serikali kupitisha sheria zinazotaka kuona walemavu wanaajiriwa kwa mujibu wa sifa, lakini bado kipo kikwazo kikubwa kwa kundi hilo kuajiriwa.

"Tumepitisha sheria mbele ya Baraza la Wawakilishi kuona walemavu wanaajiriwa katika nafasi ambazo watakuwa wakizimudu kwa kuzingatia sifa na vigezo, lakini agizo hilo halijatekelezwa," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdilatif Jussa, aliitaka serikali kutekeleza sheria zake na maagizo kuona jamii ya watu wenye ulemavu wanapata ajira serikalini kwa kazi ambazo wanazimudu.

Alisema wapo watu wenye ulemavu waliohitimu kuanzia elimu ya shahada ya kwanza katika vyuo nchini, lakini hawana ajira, huku wakihangaika na kuomba nafasi katika "Tunakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira kwa watu wenye ulemavu ambapo takwimu zilizopo haziridhishi za ajira kwa kundi hilo kutoka serikalini," alisema.

Naye Mwakilishi wa Viti Maalum, Mwantatu Mbaraka Khamis, aliitaka idara ya watu wenye ulemavu kukamilisha usajili wa watu hao pamoja na sifa za vijana ikiwamo elimu.

Aidha, aliitaka idara hiyo kuhakikisha inafuatilia zaidi na kubaini mapungufu yaliopo, na kuyafanyia kazi likiwamo suala la tatizo la ajira kwa watu wenye ulemavu serikalini.

"Idara ya watu wenye ulemavu imepewa majukumu makubwa ya kusimamia jamii hiyo, ambapo suala la uratibu kwa kundi hilo linatakiwa kuzingatiwa na kushughulikiwa kikamilifu ikiwamo suala la ajira," alisema.

Baraza la Wawakilishi limepitisha sheria ya watu wenye ulemavu na haki sawa nambari 9 ya mwaka 2006 ambapo miongoni mwa kazi zake kushughulikia haki wanazostahiki kundi hilo, likiwamo suala la ajira.

# 'Corona haitaahirisha uchaguzi mkuu 2020'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema hakuna mpango wa kuahirisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu 2020, licha ya kuwapo kwa ugonjwa Covid 19.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, alisema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti hiyo, ambapo suala la kufanyika kwa uchaguzi mkuu lilizingumziwa na wajumbe wengi waliotaka kupata ufafanuzi zaidi kutokana na kuwapo kwa janga la corona.

Aboud alisema matarajio ya serikali ni kuona kasi ya ugonjwa wa corona inapungua na hatimaye kudhibitiwa, lakini hata kama maambukizo yataendelea, uchaguzi mkuu utafanyika kwa kufuata masharti ya wataalamu wa afya ya tahadhari.

Aidha, aliwahakikishia wajumbe wa baraza hilo kwamba fedha za kusimamia uchaguzi mkuu zipo, na maandalizi yamefikia hatua nzuri, kwa mujibu wa masharti na Sheria za Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

"Nataka niwahakikishia nyinyi na wananchi kwa ujumla kwamba uchaguzi mkuu wa mwaka huu 2020 upo, na hakuna mpango wa kuahirishwa kwa sababu ya hofu ya ugonjwa wa corona...hata fedha za kufanya uchaguzi huo zipo," alisema.

Alieleza kuwa baadhi ya nchi za Afrika zimefanya uchaguzi wake katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona kwa kuzingatia masharti ya wataalamu wa afya.

Kadhalika, aliwahakikishia wananchi kwamba kila mtu mwenye sifa ya kupiga kura atatekeleza azma hiyo ikiwamo kuandikishwa katika daftari la kudumu la wapigakura.

Alisema kazi za uandikishaji wapigakura katika daftari la kudumu la wapigakura pamoja na kuhakikiwa zimefanyika.

Pia, alisema hakuna atakayeachwa katika zoezi la uandikishaji wa wapigakura katika daftari la kudumu la wapigakura, kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha uchaguzi mkuu unakuwa huru na haki.

"Serikali inapenda kuwajulisha wananchi wake kwamba hakuna mtu atakayeachwa katika daftari la kudumu la wapigakura na kukosa haki ya kushiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020," alisema.

ZEC ipo katika maandalizi ya uchaguzi mkuu ambao utahusisha uchaguzi wa rais, wawakilishi na madiwani.



Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, Simai Mohamed Said (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Yusuf Makame, kuhusu athari za mafuriko katika maskani ya Jongwe, baada ya kutembelea eneo hilo juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**.

# Wawakilishi wataka usimamizi mpango kunusuru kaya masikini

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya viongozi wakuu wa kitaifa, imeitaka serikali kusimamia vizuri mpango wa kunusuru kaya maskini, yakiwamo matumizi ya fedha.

Imetaka watu wenye sifa na vigezo ndiyo wanaopaswa kuingizwa katika utekelezaji wake.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Panya Ali Abdallah, alisema hayo wakati akiwasilisha maoni ya kamati yake katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020-2021.

Alisema mpango wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), walengwa wake ni watu wenye mahitaji, ambao ni maskini ili waweze kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Alisema hayo ndiyo malengo makubwa ya mpango wa kunusuru kaya maskini ambao ulianza tangu mwaka 1998, hivyo yasipotoshwe na kukwamishwa na watu wachache kwa maslahi yao binafsi.

Alisema kamati imetaka suala la matumizi ya fedha liratibiwe vizuri kuona fedha zilizotengwa zinawafikia walengwa, na watu ambao hawana sifa wasiruhusiwe kuingizwa katika orodha wa watu wanaostahiki kusaidiwa kwa fedha za Tasaf.

Aidha, alisema wapo watu walilipwa fedha za Tasaf wakati hawakustahiki, na ni kinyume cha utaratibu, hivyo kuharibu sifa ya Zanzibar katika kutekeleza mpango wa Tasaf.

"Tumeshuhudia katika awamu za Tasaf zilizopita matumizi ya fedha za walengwa hayakutumika vizuri, ikiwamo kuingizwa walengwa hewa...tunaomba ofisi ya kuratibu shughuli za Tasaf kuhakikisha matumizi ya fedha yanadhibitiwa," alisema.

Wakati akichangia bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020-2021, Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema hakuna mtu atakayeachwa katika mpango wa Tasaf kwa kuwa lengo ni kunusuru kaya maskini.

Mpango huo unatarajiwa kutumia Sh. 21,597,995,338, huku serikali zote mbili zikichangia pamoja na washirika wa maendeleo.

Jumla ya shehia 388 zinatarajiwa kufikiwa tofauti na kaya 206 zilizotekelezwa katika awamu zilizopita.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURiYA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi NA. 21/2020

Ombi la MOHAMEDI IDDI CHOYA KUTEULIWA kuwa Msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHANI IDD CHOYA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 08-05-2020 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 25/03/2020

157347

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**SHINYANGA**
**RUFAA YA ARDHI NA. 13 YA 2019**

**(Asilia shauri la ardhi na.143 ya 2017 katika baraza la ardhi na nyumba Wilaya ya kahama)**

**SCOLASTIKA MISANA..................MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**1. WILSON DOTO**
**2. MARKO DOTO**
**3. NGAILE DOTO............................WAJIBU RUFAA**
**4. SESILIA DOTO**

**KWA: 1. WILSON DOTO**
**2. MARKO DOTO**

**TAARIFA YA KUITWA SHAURINI**

Unajulishwa kwamba mnamo tarehe 17/06/ 2020 saa 3:00 asubuhi Shauri tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. Jaji E.Y.Mkwizu.

Hivyo unaamriw kuhudhuria siku hiyo mbele ya Mahakama kuu Shinyanga bila kukosa. Endapo hutahudhuria rufaa hiyo itasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya mahakama leo tarehe 29/04/2020.

157341

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Yohakimu Galiwusa Mbwale** anatangaza kupotea kwa cheti cha **Bachelor of Science in Engineering** chenye namba **1849/T.84** kilichotolewa na Chuo kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1988.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/KJ/RB/355/2020**

157338

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMERITECH GROUP COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 494 BCZ - BOXER 150.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/MAG/RB/357357/2020.

157339

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**THOBIUS NGONYANI LYANDER anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC 553 AUS - TVS BAJAJ.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**

**DAR/MAG/R-B/357349/2020.**

157340

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHRISTIAN RUTAIHWA MUGELE** AMEPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISH CANTER LENYE NAMBA ZA USAJILI T421 DJK, INJINI NA. 4D35G89988 NA CHESIS NA. FE638G533746.

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU AWASILIANE NAYE KWA NAMBA 0786-.418957.

AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA RB NA.
**KAG/BUK/RB/360893/2020.**

157342

---

**IN THE DISTRICT DELEGATE OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATIONCAUSE**
**NO.25.2020**
**In the matter of the Estate of the LATE ANDREW DAUDI MWANGELA**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by PENINA MTEMI LUCAS**

**GENERAL CITATION**
(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 28/05/2020.

Dated at Dodoma this 15 day of 04/2020
Petitioner
Presented for filling this 08/04/2020

157346

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**DODOMA WILAYA DODOMA MJINI**

**MADAI NAMBARI 66/2020**
**MDAI SUED AMAN LEMA**
**MDAIWA DUSTAN EMMANUEL**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwambaTsh. 500,000.

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 12/5/2020 saa mbili asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama haukuhudhuria siku tajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kuwa umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kwa kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 24/4/2020

157343

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 62/2020**

Ombi **MOHAMED ABOUD MOHAMED** kuteuliwa

Msimamizi wa mirathi marehemu **ABOUD MOHAMED ABOUD**

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/5/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 05/05/2020

157347

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(MCA/84)

Mahakama ya Mwanzo ya Kawe
Wilaya ya Kinondoni Kinondoni
MADAI NAMBARI 114 ya 2019
Mdai Frank Festo Kissima
Amdai

Mdaiwa: Bhani Cargo Hauliers
Kwa: Bhanji Cargo Hauliers wa Dsm

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/Eleza hapa habari ya madai

Utekelezaji wa Hukumu.
Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 11/6/2020 saa 2.30 Asubuhi/Alasiri kwa kujibu madai haya. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wake/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa hati hii, itaweza kutoa hukumu kuwa hati hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 7/5/2020.

1157345

---

## TANGAZO



**BW. EDSON MCHOMBA,**
KATIKA PICHA HAPO JUU, SI MUAJIRIWA/MFANYAKAZI KATIKA KAMPUNI YA **PRASAVVATJO TANZANIA LIMITED-P J T L** ILIYOPO MKOANI KILIMANJARO. AMESITIISHWA KAZI KUANZIA APRIL 1,2020. KWA YEYOTE ATAKAYEWASILIANA NAE KWA MASUALA YOYOTE YA KIBIASHARA YANAYOHUSIANA NA KAMPUNI YA PJTL AU MASUALA MENGINE, ITAKUA NI KWA MATAKWA YAKE BINAFSI. KAMPUNI YA PRASAVVATJO TANZANIA LIMITED HAITAHUSIKA KWA LOLOTE/CHOCHOTE KITAKACHOHUSISHWA NA MUHUSIKA ALIYETAJWA HAPO JUU.

TUNAPENDA KUWATAHADHARISHA WATEJA WETU WOTE KUWA MAKINI.

**PRASAVVATJO TANZANIA LIMITED,**
**P,O BOX 6847, MOSHI, KILIMANJARO**

157352

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
CIVIL CASE NO 61 OF 2019
MARTINI ORDUNYI LUKUMAY ............PLAINTIFF

VERSUS
INSP .PAZIA & ANOTHER ..................DEFFENDANT

**NOTICE OF MENTION**

TO INS. PAZIA
INS HASSAN

**TAKE NOTICE** thatthe above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's court of Arusha at Arusha on the 14th day of MAY 2020 at 8:30 am o'clock in the forenoon, before Hon M.J. MAHUMBUGA – RM .

You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** That in default of your appearance on that day tine before mention or hearing the court may proceed in your absence.

Given under my hand the seal of the court this 28th day of **APRIL 2020.**

157349


NIPASHE NI JIBU






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Profesa mtafiti corona auawa Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MAUAJI ya raia wa China, ambaye ni mtafiti wa masuala ya virusi vya corona kwenye ardhi ya Marekani yamesababisha sintofahamu.

Mtafiti huyo, Prof. Bing Liu, mwenye miaka 37 kutoka katika Chuo Kikuu cha Tiba cha Pittsburgh, Marekani alikutwa amefariki nyumbani kwake siku ya Jumamosi.

Wenzake walisema alikuwa karibu kupata matokeo muhimu ya utafiti kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona, tukio lililosababisha kuwapo kwa maoni mitandaoni yanayoeleza kuwa yawezekana Prof. Liu aliuawa, lakini polisi wanasema ni tukio la kujiua.

**hakuna ushahidi wa kuhusisha tukio hilo na utafiti wa Prof.Liu na mazingira ya sasa ya changamoto za kiafya.**

### KWA NINI LIU ALIUAWA?

Prof. Liu alikutwa akiwa na majeraha mengi ya risasi kichwani, shingoni katika eneo la Pittsburgh yalipo makazi yake kwa mujibu wa polisi wa eneo hilo.

Mtu aliyekuwa na silaha alitambulika kuwa na miaka 46, mhandisi wa programu ya kompyuta, Hao Gu. Mamlaka zinasema muuaji naye alijiua baada ya kurudi kwenye gari lake.

Taarifa kutoka polisi zinaeleza kuwa Prof. Liu na Gu walikuwa wanafahamiana.

Uchunguzi umebaini kuwa lilikuwa tukio la kuua na kujiua lililotokana na mgogoro wa muda mrefu wa masuala ya kimapenzi.

Wamesema hakuna ushahidi wa kuhusisha tukio hilo na utafiti wa Prof. Liu na mazingira ya sasa ya changamoto za kiafya.

### LIU NI NANI?

Marafiki wa Prof. Liu wamemwelezea alikuwa ni mtafiti wa kipekee ambaye alikuwa ukingoni kufanikisha kupata matokeo muhimu ya kuelewa maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Waliomboleza kifo cha Prof. Liu na kuahidi kumalizia utafiti wake zikiwa ni juhudi za kuenzi ubora wake katika uwanja wa kisanyansi.

Prof. Liu, raia wa China alipata shahada yake ya kwanza na shahada ya uzamivu katika masomo ya sayansi ya kompyuta nchini Singapore kabla ya kufanya utafiti nchini Marekani.

Aliwahi kuungana na wanabaiolojia wengine kufanya utafiti kuhusu kinga ya binadamu, kwa mujibu wa wasifu wake mtandaoni. **BBC**



Wanafunzi wakiwa darasani katika mji wa Wuhan, China. **PICHA: REUTERS**

## Vurugu zatawala kampeni uchaguzi

**BUJUMBURA,** Burundi

VURUGU zimejitokeza wakati wa kampeni za uchaguzi nchini Burundi.

Mfuasi mmoja wa chama cha upinzani CNL ameuawa na wengine wanane kujeruhiwa katika makabiliano ya mapanga na vijana wa Imbonerakure wa chama tawala, CNDD-FDD.

Mwanasheria Mkuu, Sylvestre Nyandwa, aliwaonya wanasiasa kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria iwapo watasababisha usalama kuharibika.

Akiwahamasisha wafuasi wa chama chake, Kathy Nkezimana, mgombea ubunge kwa tiketi ya chama cha upinzani CNL, aliyekamatwa na kufungwa jela muda mfupi baada ya kuendesha kampeni katika tarafa ya Mugongomanga mkoani Bujumbura vijijini, alisema kamwe hawatowasahau watu waliouawa.

Kufungwa kwa mgombea huyo kumefuatia makabiliano ya kutumia mapanga kati ya wafuasi wa chama CNL na vijana Imbonerakure wa chama CNDD-FDD, ambapo mfuasi mmoja wa chama cha CNL aliuawa na wengine wanane kujeruhiwa katika tarafa ya Ntega mkoani Kirundo kaskazini mwa nchi. **DW**

## UN yataka mabilioni yaelekezwe nchi maskini

**WASHINGTON,** Marekani

UMOJA wa Mataifa (UN) unaendelea kuhimiza mchango wa mabilioni ya dola kwa ajili ya msaada wa kupambana na virusi vya corona kwa nchi maskini duniani.

Mkuu wa Masuala ya Kibinadamu wa UN, Mark Lowcock, alisema fedha hizo ni muhimu kuokoa mamilioni ya maisha ya wanadamu na kusaidia kuzuia kuenea kwa virusi hivyo katika nchi zisizokuwa imara.

Alisema nchi maskini duniani hazitegemewi kufikia kilele cha maambukizi ya corona mpaka baada ya miezi mitatu au sita.

Alisema tayari nchi hizo zinashuhudia ukosefu wa ajira na kipato, pamoja na mgawanyo finyu wa mahitaji ya chakula na watoto wakiwa hawapati chanjo za kawaida.

Alisema ombi la awali lilikuwa kupata ufadhili wa dola bilioni mbili, na shirika hilo limesema linahitaji dola bilioni 6.7.

"Iwapo hatutawasaidia watu maskini sana - hasa wanawake na wasichana na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatari - wakati wakikabiliana na janga hili na athari za kudorora kwa uchumi wa dunia, sote tutakuja kukabiliana na athari zinazotokana na janga hili kwa miaka mingi inayokuja," alisema Lowcock.

Alisema ombi hilo la msaada linaloendelea linajumuisha nchi tisa kwenye orodha ya mataifa yaliyo katika hatari zaidi; Benin, Djibouti, Liberia, Msumbiji, Pakistan, Ufilipino, Sierra Leone, Togo na Zimbabwe.

Alisema nchi kadhaa tayari zimeanza kulegeza masharti ya kutotoka nje yaliyokuwa yamewekwa kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo kwa kipindi cha miezi michache iliyopita.

Lakini wataalamu wa afya wanaonya kuwa kuna uwezekano wa maambukizi hayo kuibuka tena iwapo amri hizo za kutotoka nje zitaondolewa kwa haraka.

"Tunajiaminisha kuona maambukizi yakirejea tena ambayo hatutaweza kuyahimili," alisema Dk. Ian Lipkin wa Chuo Kikuu cha Columbia, New York.

Serikali za Ulaya na baadhi ya majimbo ya Marekani ni miongoni mwa sehemu ambazo zimeruhusu aina ya biashara kufunguliwa tena, na kuruhusu watu kwenda kwenye migahawa na madukani, lakini kwa sharti la kuepuka misongamano na kutokaribiana na watu wengine.

Hadi kufikia jana watu milioni 3.8 waliopimwa na kuthibitishwa kuwa na maambukizi ya virusi vya corona duniani kote, wakati idadi ya vifo ikifikia 264,000. **VOA**

# KIUNGO MAN CITY AIMWAGIA SIFA LIVER



**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester City, Rodri ameisifia Liverpool kuwa na msimu wa "kuvutia" kwenye Ligi Kuu England.

Kikosi hicho cha Jurgen Klopp, kilikuwa kinaongoza kwa pointi 25 kileleni mwa msimamo wakati ligi iliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona Machi, mwaka huu.

City walikuwa kwenye nafasi nzuri ya kulitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu tangu mwaka 1990.

Rodri amekisifia kikosi hicho cha Klopp, ambacho kimeshinda mechi 27 kati ya 29 za Ligi Kuu msimu huu.

"Wakati mwingine soka lipo kama hivi. Liverpool wamekuwa na msimu wa kuvutia wa ligi," amesema mchezaji huyo raia wa Hispania akinukuliwa na Sky Sports.

"Walijipanga kwa ajili ya msimu mzima wa ligi, na kwa hakika kabisa walikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi na hakuna kilichokuwa kinaonekana kinaweza kuwazuia.

"Lakini sisi tulikuwa na matatizo mengi mwaka huu. Tulikuwa na wachezaji wengi majeruhi na ambao walikuwa muhimu kwa timu, lakini haukuwa msimu mbaya sana kwetu kwa sababu tupo nafasi ya pili."

# *Maguire afunguka kilichoigharimu United*



**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire anaamini kutoimarika kwa kiwango cha Manchester United ni moja ya tatizo kubwa msimu huu kwa kikosi hicho.

Wakati msimu uliposimamishwa kutokana na virusi vya corona Machi, mwaka huu, United walikuwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, lakini bado wapo kwenye Ligi ya Europa na Kombe la FA.

Vijana hao wa Ole Gunnar Solskjaer waliifunga Manchester City na Chelsea mara mbili kwenye ligi, pamoja na Tottenham, lakini waliachwa pointi na Aston Villa, Watford, Bournemouth na West Ham.

Nahodha huyo wa United, Maguire amesema timu yao imekuwa na kiwango kisichoendelea na kuwaweka kwenye wakati mbaya zaidi msimu huu.

"Pengine mpinzani wetu mkubwa ni sisi wenyewe. Naweza kusema kama timu kiwango chetu haijaimarika, na kukosa mwendelezo, kwani kuna wakati tunakuwa bora na wakati tunakuwa ovyo," amesema wakati akijibu kipindi cha maswali na majibu kutoka kwa mashabiki kupitia tovuti ya klabu hiyo.

"Kuna wakati tumekuwa bora kwenye mechi zetu, halafu tunakuwa ovyo na kufungwa kirahisi sana. Hivyo nasema mpinzani wetu mkubwa ni sisi wenyewe. Tunatakiwa kuwa imara kwa akili na nguvu.

"Tulikuwa kundi la wachezaji vijana, lakini hatutumii hicho kama ndio kigezo cha kufanya vibaya. Tunataka kuwa vijana na kucheza kama tuliopevuka."

## Eriksen asaka namba ya kudumu Inter

**MILAN,** Italia

CHRISTIAN Eriksen anataka kujiimarisha yeye mwenyewe pale Inter Milan wakati msimu utakapoanza tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Eriksen alijiunga na Inter akitokea Tottenham Januari mwaka huu, lakini alicheza mechi nane tu kabla ya msimu kusimamishwa kutokana na ugonjwa wa COVID-19.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alianza katika mchezo mmoja tu wa Serie A kwa Inter, ambao walikuwa nafasi ya tatu kwenye msimamo.


Eriksen mwenye umri wa miaka 28, sasa anataka kucheza mara kwa mara kwa Inter, akiwa amesaini mkataba wa miaka minne na nusu kukaa klabuni hapo.

"Napenda kucheza soka," aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa Instagram wakati alipokuwa akiulizwa maswali na Dkt. Sporten.

"Hiyo itakuwa hamasa kubwa kwangu. Lengo langu ni kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara Inter."

Alipoulizwa kama kweli anatakiwa kuondoka Inter, Eriksen alijibu: "Hapana, kwa hakika kabisa."

Klabu nyingi za Ligi Kuu Italia, Serie A, zinarudi kwenye mazoezi ya wiki hii wakati wakijiandaa kuendelea na msimu.



HABARI MICHEZO

# Herrera ahuzunishwa na ubingwa wa PSG

**PARIS,** Ufaransa

ANDER Herrera amebainisha huzuni yake namna Paris Saint-Germain ilivyoshinda taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, na amekubali kwamba, hakupanga kuondoka Manchester United.

Herrera amesema alikuwa na mtazamo tofauti na bodi ya United kabla ya kuondoka Old Trafford kujiunga na miamba hao wa soka la Ufaransa akiwa mchezaji huru.

Wakati mitaa ya jiji la Paris ikiwa imepambwa na wachezaji wa kizazi cha dhahabu chini ya umiliki wa kampuni tajiri kutoka Qatari, Herrera hajafurahishwa na namna ligi hiyo ilivyomalizika.

Kama ilivyokuwa kwenye Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, ilifutwa msimu huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

PSG ambayo ilikuwa kileleni mwa msimamo ilitawazwa kuwa mabingwa, lakini kiungo wa huyo wa kimataifa wa Hispania, Herrera hajafurahishwa na hilo.

"Nikiwa mkweli, sikusherehekea," amesema Herrera akiiambia ESPN. "Napenda soka, lakini napenda kucheza soka na kushinda mataji dimbani."

Mchezaji huyo wa zamani wa Athletic Bilbao aliongeza: "Natumaini tutaweza kupigania mataji mengine ambayo bado tunatakiwa kucheza uwanjani tukiwa na mashabiki uwanjani na ngoja tuone kama tunaweza kupambana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nikiwa mkweli, kwa hakika ni huzuni kushinda taji langu la kwanza kwa staili hii."

Herrera alishinda taji la FA, EFL na Ligi ya Europa akiwa na United, lakini katika miaka yake mitano ya kukaa pale Manchester hakuweza kubeba taji la Ligi Kuu.

Amezungumzia furaha yake ya "uhusiano mzuri" na Makamu Mwenyekiti Mtendaji Mkuu wa United, Ed Woodward, lakini hakutosha kumbakiza yeye England.

Muda mfupi baada ya kujiunga na PSG, Herrera alielezea kulikuwa na kutokuelewana kati yake na bodi ya United na hivyo akakubali kwenda Ufaransa.





# FIFA YACHUNGUZA USAJILI WA FERNANDES

**MANCHESTER,** England

USAJILI wa Bruno Fernandes kwenda Manchester United kutoka Sporting CP unachunguzwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), baada ya Sampdoria kufungua madai dhidi ya klabu ya Ureno.

Madai ya Sampdoria yanahusiana na malipo ambayo wanaamini wao walitakiwa kulipwa katika ada ya awali ya Fernandes ya pauni milioni 48 kwenda Old Trafford Januari mwaka huu.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno alijiunga na Sporting kutoka Sampdoria kwa ada ya euro milioni 8.5 Juni mwaka 2017.

Madai ya Sampdoria yanaihusisha Sporting peke yake, maana yake United haina kosa lolote katika usajili huo.

Katika taarifa yake, Fifa ilisema: "Tunathibitisha kwamba, Aprili 3, mwaka 2020 Klabu ya Italia, UC Sampdoria, ilileta malalamiko kwa Fifa dhidi ya klabu ya Ureno, Sporting kuhusu sheria za mikataba inayohusu usajili wa mchezaji wa Ureno, Bruno Miguel Borges Fernandes.

Gazeti la The Times lilidai kwamba, Sampdoria wanatakiwa kulipwa euro milioni 4.65 kwa mauzo ya Fernandes kwa sababu alikuwa na kipengele kwenye mkataba wake wa kiasi cha fedha cha kumwachia wakati akihamia Lisbon ambacho hakikulipwa wakati huo.

# *Boateng ataka kumalizia soka Bayern Munich*

**MUNICH,** Ujerumani

JEROME Boateng anapenda maisha ya pale Bayern Munich chini ya Hansi Flick na atakuwa na furaha kuendelea kucheza hapo katika kipindi kilichobaki kwenye mkataba wake.

Beki huyo wa kati amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwenye dimba la Allianz Arena wakati wa dirisha lijalo la usajili, lakini amekuwa na maelewano mazuri na Flick, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo Novemba mwaka jana kama kocha wa muda.

Mkataba wa sasa wa Boateng unamalizika mwaka 2021 na alionekana kama asingemaliza muda huo hapo, lakini Flick alipoichukua Bayern amekuwa akichezesha mara kwa mara tofauti na ilivyokuwa kwa kocha Niko Kovac aliyefukuzwa.

"Namwelewa sana Hansi Flick. Kama asingekuwa kocha sasa, nisingekuwapo hapa FC Bayern," amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 akiliambia gazeti la Sport Bild.

"Mkataba wangu na Munich unamalizika 2021 na naweza kukamilisha ndoto zangu chini ya Hansi Flick.

"Najua kwamba, klabu hii imefanya mengi kwangu, kama ambavyo mimi nimeifanyia. Klabu hii itabakia kuwa kwenye moyo wangu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED, CHELSEA TOTTENHAM VITANI

## Ni katika mbio za kuwania saini ya kiungo Mserbia wa Lazio ambaye dau lake ni...

**LONDON,** England

MANCHESTER United, Chelsea na Tottenham zimewashiwa taa nyeupe katika kukamilisha mchakato wa kumsajili, Sergej Milinkovic-Savic, lakini Lazio imeweka wazi ili kuruhusu nyota huyo kuondoka klabuni kwake, inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 80.

**Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Serbia, ambaye ana umri wa miaka 25, amekuwa kwenye rada za klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu England kwa muda mrefu lakini Lazio ilikuwa ikishikilia msimamo wake wa kutomuuza nyota huyo.**

Lakini kwa mara ya kwanza, Mkurugenzi wa Michezo, Igli Tare, amekiri wakati umefika sasa kwa Milinkovic-Savic kufanya uamuzi kuhusu hatima yake kama anataka kuondoka Stadio Olimpico.

Tare aliulizwa na Sky Sport Italia nini kitatokea kama Lazio itapokea kiasi cha fedha ambacho imetajwa cha kumuuza Mserbia huyo.

Kiongozi huyo alisema: "Uamuzi utakaofanywa na mchezaji ndio muhimu. Kwa ujumla ninaweza kusema kama mchezaji atakachofikiria itakuwa ni juu yake kubakia au kuondoka kuelekea mahali kwingine, haitakuwa tatizo.

"Amefikia mwisho wa ngwe yake. Hebu angalia kilichotokea kwa Napoli msimu huu. Ukweli ni kwamba alikaa Rome kwa muda wa miaka mitano kwa sababu alikuwa na mahusiano imara kati ya klabu na jiji hilo."

Tare aliongeza: "Wakati kunapokuwa na changamoto katika upande wetu, huwa hatuchukui uamuzi wa moja kwa moja. Hata hivyo, mambo hujadiliwa na kufanyiwa tathmini inapofika mwishoni mwa msimu."

Kwa muda mrefu Kocha wa Tottenham, Jose Mourinho, alikuwa anavutiwa na kiwango cha mchezaji huyo na mwaka 2018 alikuwa anataka kumsajili wakati alipokuwa anaifundisha Manchester United.

Mserbia huyo ambaye jina lake maarufu ni 'Sergeant' kwa sababu ya kuwa na nguvu zaidi, uwezo wa kuongoza wenzake na kuonyesha ufundi anapokuwa na mpira, anatajwa huenda akachukua mikoba iliyoachwa na Christian Eriksen katika kikosi cha Spurs.

Kocha wa Chelsea, Frank Lampard naye ni shabiki wa mchezaji huyo, wakati Ole Gunnar Solskjaer anamwona Mserbia huyo anaweza kuwa mrithi wa Paul Pogba endapo kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa ataondoka Manchester United.

Milinkovic-Savic pia anatajwa kuhusishwa na mipango ya kujiunga na Juventus na Inter Milan zote zinazoshiriki Serie A, lakini mchezaji huyo ameweka wazi hataki kujiunga na timu hizo ambazo ni wapinzani halisi wa Lazio.

Nyota huyo ambaye amefunga mabao 36 na kutoa pasi za mwisho za magoli 26 katika mechi 194 alizoichezea Lazio, alisajiliwa kwa dau la pauni milioni 16.2 kutoka Genk ya Ubelgiji mwaka 2015 na Lazio itatengeneza faida kubwa endapo itafanikiwa kumuuza.

## ZISIKUPITE

### IGHALO MAMBO SAFI

MABOSI wa Manchester United wanataka kumwongeza mkataba wa mkopo straika wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Odion Ighalo (30), ambaye walimsajili akitokea Shanghai Shenhua. ***(Standard)***

### JORGINHO KUREJEA JUVE

JUVENTUS iko katika mazungumzo na wawakilishi wa Jorginho ili kukamilisha mchakato wa kumrejesha klabuni hapo kiungo huyo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Italia ambaye ana umri wa miaka 28. ***(National)***

### KURZAWA ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inapata matumaini ya kumnasa beki wa kushoto wa Ufaransa, Layvin Kurzawa akitokea Paris St-Germain baada ya Barcelona kusitisha nia ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Le10 Sport - in French)***

### MEUNIER AKARIBIA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inaongoza katika mbio za kuwania saini ya beki wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Thomas Meunier, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(Le Parisien - in French)***

### RASHICA AGOMBEWA

LIVERPOOL, Southampton na RB Leipzig ziko vitani kuwania saini ya winga wa Werder Bremen, Milot Rashica (23), nyota huyo raia wa Kosovo anatarajia kumaliza mkataba wake na klabu hiyo ya Ujerumani ifikapo Juni, mwaka huu. ***(Bild - in German)***

### UNITED YAMGANDA GOMES

MANCHESTER United imempa ofa ya mshahara wa pauni 30,000 kwa wiki mshambuliaji wake, Angel Gomes (19), ili kumshawishi asiondoke kama mchezaji huru katika majira ya joto na ikionyesha bado ina mipango naye licha ya kuonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Birmingham City, Jude Bellingham (16). ***(Sun)***

### UNITED, ARSENAL VITANI

MANCHESTER United imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Sunderland, Joe Hugill (16), ambaye pia anawindwa na Arsenal, Spurs, Wolverhampton Wanderers na Leeds United. ***(Northern Echo)***

### BAKAYOKO KURUDI MILAN

KIUNGO wa Chelsea Mfaransa, Tiemoue Bakayoko, ambayo kwa sasa yuko kwa mkopo Monaco, ameweka wazi nia yake ya kurejea AC Milan. Nyota huyo ambaye ana umri wa miaka 25, msimu wa 2018/19 aliichezea kwa mkopo klabu ya San Siro. ***(Calciomercato - in Italian)***

### LIVERPOOL, CITY VITANI

LIVERPOOL na Manchester City zimeonyesha nia ya kuwania saini ya kiungo chipukizi wa KV Mechelen, Aster Vranckx ambaye ni raia wa Ubelgiji na ana umri wa miaka 17. ***(Mirror)***

### KAMARA KUIKAMUA CITY

MANCHESTER City inajiandaa kutoa dau la pauni milioni 28 ili kufanikisha usajili wa beki Mfaransa wa Marseille, Boubacar Kamara, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Le10 Sport - in French)***

HABARI MICHEZO

# MGOSI ATABIRI MAKUBWA KATIKA LIGI YA WANAWAKE

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema licha ya changamoto mbalimbali zilizoko katika Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, anaamini ligi hiyo itakuwa bora zaidi ndani ya miaka miwili ijayo.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mgosi, alisema anafahamu programu zilizoandaliwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na endapo zitafuatwa kikamilifu, kiwango na maendeleo ya soka la wanawake yatapatikana.**

Mgosi alisema kuwa mwamko wa soka la wanawake hapa nchini ni mkubwa na Tanzania ikiandaa tena mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (U-17 na (U-20), itasaidia kuongeza mwamko.

"Changamoto kubwa ni namna ya uendeshaji wa timu zinazoshiriki katika Ligi ya Wanawake na uhalisia, ila ninaamini kwa programu zilizoandaliwa na TFF, ndani ya miaka miwili, ligi hii itakuwa mbali na tutaendelea kufanya vema katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati," Mgosi alisema.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba alisema anatarajia kuona ushindani ukiongezeka katika Ligi Kuu ya Wanawake na ujio wa Yanga Princess na Ruvuma Queens umesaidia kuongeza mvuto kwenye ligi hiyo.


"Suala la viwanja limekuwa ni changamoto, ligi imekuwa ikichezwa kwenye viwanja ambavyo havina mvuto, ila kwa upande wa wanawake tumeona vipaji, lakini kwa soka la vijana la wanaume wanaamini wanajua zaidi," Mgosi alisema.

Aliongeza kuwa ili maendeleo katika soka la wanawake yaongezeke ni lazima uwekezaji uboreshwe, huku viongozi na wasimamizi wa mpira wakitakiwa kufuata weledi katika kutimiza majukumu yao.

"Ni mpira wa wanawake na tunasema waamuzi wake wanawake, ninashauri tutumie marefa wanaume huku tukiendelea kuwapika waamuzi wanawake ambao baadaye wataendelea kusimamia ligi yao," alisema Mgosi.

Alisema kama changamoto ya udhamini katika Ligi Kuu ya Wanawake itaendelea, anashauri ligi hiyo kwenye hatua ya awali ichezwe kwa kanda na baadaye timu zitakazofanya vizuri zitakutana katika kituo kimoja ili kusaka bingwa wa msimu husika.

MAZOEZI...




Bondia, Mike Tyson (kushoto), akiwa na mkufunzi wake, Rafael Cordeiro ambaye anamwongoza katika mazoezi ili kuimarisha kiwango chake, huku kukiwa na tetesi za mkongwe huyo kurejea ulingoni. **PICHA: MTANDAO**

# JKT Tanzania yafikiria mbele

**Na Saada Akida**

HUKU wakisubiri taarifa rasmi kuhusu hatima ya msimu wa 2019/20 wa Ligi Kuu Bara, uongozi wa JKT Tanzania umeshaanza maandalizi ya kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema wamejipanga kufanya mabadiliko katika kikosi chao na hiyo inalenga kuiboresha timu yao.

Nyumba alisema mabadiliko ya kikosi hiyo yatafanywa kwa kufuata mapendekezo yatakayotolewa na benchi la ufundi la timu hiyo kwa kuzingatia mapungufu waliyoyabaini ndani ya msimu huu.

"Tunahitaji kumaliza msimu huu katika nafasi nzuri, lakini tunatarajia kuboresha timu yetu kwa kuhakikisha tunafanya vizuri zaidi ya msimu huu," alisema Nyumba.

Kiongozi huyo alisema wameshafahamu walipokosea msimu huu na kwa 'kuyabeba' mapungufu hayo, watahakikisha hawarudii makosa katika msimu mpya.

"Hatutaki kuona tunarudia tena makosa, katika msimu mpya tunajipanga kupambana kumaliza kwenye nafasi tano za juu, hiyo ndiyo mipango yetu," alisema Nyumba.

Alisema watahitaji kuanza vizuri na hata kumaliza vizuri msimu tofauti na hali ilivyokuwa katika msimu huu ambao walianza kwa 'kusuasua' katika baadhi ya michezo ambayo iliwaweka kwenye hatari.

## Riadha D'Salaam watakiwa kuamka

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wa Timu ya Riadha ya Mkoa wa Dar es Salaam wamekumbushwa kuongeza nidhamu ili wafikie malengo yao licha ya kuwapo kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Kocha wa timu hiyo, Idd Muhunzi, aliliambia gazeti hili endapo wachezaji hao watafuata vema programu za mazoezi walizopewa, viwango vyao vitaimarika na hakuna ambaye ataathirika na uamuzi wa kusimamisha mazoezi ya pamoja.

"Nashauri wachezaji wazidishe nidhamu, mchezaji mzuri ni yule mwenye nidhamu pamoja na kufuata maelekezo anayopewa na mwalimu wake," alisema Muhunzi.

Kocha huyo alisema kikosi chake kiko tayari kushiriki mashindano yoyote watakayoalikwa kwa sababu wanariadha wake wako kwenye viwango vya juu wakati wote.

"Nimefurahi kusikia Rais wetu, John Pombe Magufuli anafikiria kurejesha michezo, ni jambo jema, tunapaswa kucheza huku tukiwa na tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo," Muhunzi alisema.

## Machomanne FC kukomaa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABOSI wa Machomane FC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar wamesema wanaendelea na mikakati kuhakikisha timu yao inafanya vizuri katika mechi zilizobakia za msimu huu, endapo ligi hiyo itarejea tena.

Katibu Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Kombo, alisema wanajipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili wajiepushe na janga la kushuka daraja.

Kombo alisema wachezaji wao wanajiimarisha kwa kufuata programu za mazoezi walizopewa ili malengo yao ya kubakia kwenye Ligi Kuu Zanzibar yanatimia.

"Tunajipanga kuhakikisha timu yetu haishuki daraja, tunawakumbusha wachezaji watumie mbinu zitakazowafanya kutopoteza michezo, hususani katika kipindi hiki ambacho ligi inaelekea ukingoni," alisema Kombo.

Aliongeza anaamini ligi hiyo ikirejea, ushindani utaongezeka hasa katika mechi zinazohusisha timu zilizoko kwenye hatari ya kushuka daraja.

"Wachezaji wamekaa muda mrefu bila mazoezi, lakini viongozi tunatakiwa kuandaa bajeti za kumalizia ligi na pia tukifahamu tunaelekea katika msimu mpya ambao unahusisha gharama za usajili," Kombe alisema.

Mapema wiki hii Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), lilisema linasubiri mwongozo wa serikali kuhusiana na hatima ya ligi mbalimbali zinazosimamiwa na shirikisho hilo.

Michezo

Ijumaa Mei 8, 2020

Nipashe



United, Chelsea Tottenham vitani

UKURASA 22



Kiungo wa Simba, Jonas Mkude (kulia), akiwa na Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohammed Dewji 'Mo' baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia timu hiyo hapo mwaka jana. **PICHA: MAKTABA**

# MKUDE AIWEKA SIMBA MTEGONI

## ●●● Ni baada ya tetesi za kutakiwa na TP Mazembe ya DRC, aeleza ni habari njema...

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, Jonas Mkude, amesema bado hajapata taarifa rasmi kuhusiana na tetesi za kutakiwa na vigogo wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), TP Mazembe.

**Mapema wiki hii, mitandao mbalimbali imeandika kuhusiana na kiungo huyo kuwindwa na TP Mazembe iliyowahi kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Simba, Mbwana Samatta, ambaye kwa sasa anaitumikia Aston Villa ya England.**

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Mkude, alisema yeye bado ana mkataba na vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba hivyo hawezi kuzungumzia ofa yoyote kutoka katika timu nyingine.

Mkude alisema mpaka kufikia jana, hakuwa na taarifa kutoka kwa viongozi wake na hivyo hawezi kuzungumzia chochote kuhusiana na mchakato huo wa kutakiwa na mabingwa hao wa zamani wa Afrika, TP Mazembe.

"Bado sijapata taarifa yoyote kuhusu suala hilo, ni habari njema kwangu lakini bado nina mkataba, mimi ni mali ya Simba," alisema kiungo huyo ambaye ameitumikia Wekundu wa Msimbazi kwa miaka 10 sasa.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili klabu hiyo haijapokea ofa yoyote kutoka TP Mazembe au timu nyingine kwa ajili ya kumsajili kiungo wao.

Manara alisema endapo Simba itapokea ofa kutoka klabu yoyote duniani, itawalazimu kuitisha kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ili kujadili maombi hayo.

"Hakuna ofa yoyote iliyotufikia mezani kwetu mpaka muda huu (jana mchana) ninapozungumza na wewe, kwa sasa dunia zima tupo katika harakati za kupambana na ugonjwa wa corona, ila kama hilo jambo lina ukweli basi tunasubiri."

Manara alisema ofa yoyote itakayotua katika klabu hiyo, itajadiliwa kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili.

"Ofa itakapokuja mezani, Simba ina utaratibu wake, Bodi ya Wakurugezi itajadili na kuchukua uamuzi kwa kuangalia maslahi ya pande zote, namaanisha kwa klabu na kwa mchezaji anayetakiwa kuuzwa," alisema Manara.

Mkude amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na timu hiyo aliyoanza kuitumikia kwenye kikosi cha vijana wa umri chini ya miaka 20 (Simba B), wakati huo kikiwa chini ya Suleiman Matola.

Mbali na kuwa tegemeo katika kikosi cha kwanza cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, Mkude (27), ni kiungo tegemeo katika Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), ambayo sasa inafundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije.

## Mbelgiji Yanga abadili hesabu

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kusikia huenda Ligi Kuu Tanzania Bara ikarejea hivi karibuni, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amewatumia wachezaji wake programu mpya ya mazoezi kwa lengo la kuwaweka tayari na 'mshikemshike' wa ligi hiyo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Boniface Mkwasa alisema programu hiyo wameipokea tangu juzi na wataanza kuifanyia kazi kama ilivyopangwa.

"Jana (juzi), niliwasiliana na Luc, ameniambia ametuma programu nyingine ambayo anataka kuona wachezaji wanaendelea nayo katika kipindi hiki cha mpito, huku yeye akiwafuatilia kwa njia ya video mtandaoni," alisema Mkwasa.

Kocha huyo alisema kila mchezaji ametakiwa kufuata kwa makini maelekezo yaliyopo kwenye programu hiyo ambayo itawasaidia kuwa imara mara tarehe mpya ya kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara itakapotangazwa.

"Kocha Mkuu amesema kama kila mchezaji atafuatilia kwa usahihi, hakuna ambaye atakosa mechi wakati ligi itakaporejea, hii itawarejesha kwenye ushindani baada ya kupumzika kwa muda mrefu kutokana na kujikinga na janga la corona," Mkwasa alisema.

Aliongeza Yanga iko tayari kupokea uamuzi wowote utakaotangazwa kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Bara baada ya Rais John Pombe Magufuli, kusema anafikiria kuruhusu ligi hiyo iendelee kama kawaida.

"Kauli nimeisikia, lakini mpaka sasa sijakutana na wachezaji kwa sababu hatujaruhusiwa, nasubiri pia majibu kama Ligi Kuu itaendelea au la, ndipo niwape utaratibu mzima wa mazoezi," aliongeza Mkwasa.

Alisema wanashukuru wachezaji wao wote wako salama na hiyo inawaweka kwenye nafasi nzuri ya kuwa na kikosi kilichokamilika.

"Ni muhimu wakati huu kila mchezaji akachukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu (corona), ili pale Ligi Kuu itakapoanza, asiwepo yoyote atakayebainika na ugonjwa huo hatari ambao umeua na kuathiri watu wengi duniani," Mkwasa aliongeza.

Kuhusu mchakato wa usajili kuelekea msimu mpya, kocha huyo aliwataka wanachama na mashabiki wa Yanga kusubiri dirisha la usajili litakapofunguliwa rasmi kwa sababu sasa si kipindi chake rasmi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >